# Pambazuko

Toleo Namba 168 — Jumatatu, Juni 8-13, 2026


# Mwanga, giza bajeti mpya




- Nini kinapikwa kwa 2026/27 Uk. 6&7

**Ushirikiano Muhimu...**



*Rais Samia Suluhu Hassan akikaribishwa na Rais wa Russia, Vladmir Putin katika Ikulu ya Kremlin, jijini Moscow wakati wa ziara rasmi ya kikazi ya siku tatu nchini humo mwishoni mwa wiki. (Picha na Ikulu)*

## Yuda amechokozwa, vyema asichokozeke

YUDA wa Biblia alimsaliti Bwana Yesu. Siamini kama mleta hoja anamaanisha msalitiwa katika hoja yake ni sawa na Bwana Yesu!

Safu Uk. 10

## Tanzania kukabili dhamira ya Bunge la Ulaya



Habari Uk. 22

**Sheria**

## Jaji John Ruhangisa ashangaa sheria batili kutofutwa

Habari Uk.15

# Nini kitarajiwe ziara ya Rais Samia Russia

Uk. 12



**Jicho la Tai**

## Waafrika Kusini waache ujinga

KUNA mambo yakitokea Afrika, mtu unabaki unacheka kwa uchungu. Unajiuliza; hivi sisi Waafrika tulikosea wapi?...

Safu Uk. 5

## Vita urais 2030 yakolea CCM

Uk. 16

Tahariri

# Tamaa ya urais isitupotezee dira

KUNA dalili ambazo taifa likianza kuziona mapema, halipaswi kukaa kimya, wala kuzichekea au kuamua kuzifumbia macho. Ni lazima zikemewe mapema.

Moja ya dalili hizo kwa sasa ni mwendo unaoanza kujitokeza nchini Tanzania kwa makundi ya kisiasa kujipanga mapema mno kuhusu uongozi wa Tanzania baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kumaliza muda wake wa kikatiba mwaka 2030.

Katika demokrasia, siyo dhambi kwa mtu kuwa na ndoto ya uongozi. Siyo kosa kwa chama, taasisi au mwanasiasa kufikiri kuhusu mustakabali wa nchi. Lakini kuna tofauti kubwa kati ya maandalizi ya uongozi na minyukano ya tamaa.

Kuna tofauti kati ya kujenga hoja za taifa na kujenga makundi ya kuumizana. Kinachoanza kuonekana sasa kinapaswa kutazamwa kwa jicho la tahadhari kubwa.

Kibaya zaidi, minyukano hii inaonekana kuanza kubeba sura mbaya ya kuchafuana. Badala ya watu kujipambanua kwa uwezo, maono, uadilifu na rekodi ya utumishi, baadhi yao wanaonekana kuchagua njia ya kuharibia wenzao ili wao waonekane bora.

Hii ni siasa mbaya na isiyokuwa na maono, hatari na isiyotakiwa kupewa nafasi ya kuendelea kumea katika taifa linalohitaji utulivu, maendeleo na mshikamano.

Hili likifanyika vijiweni ni baya; likifanyika mitandaoni ni hatari; lakini likianza kuingia hadi kwenye vikao muhimu vya Bunge, linakuwa janga la kitaifa.

Ieleweke kwamba Bunge ni chombo cha wananchi. Ni mahali pa kujadili bajeti, sheria, uwajibikaji, shida za wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara, wagonjwa, wanafunzi na wananchi. Siyo uwanja wa kupima nguvu za makundi yanayotafuta mrithi wa urais miaka mingi kabla ya wakati wake.

Tanzania ina changamoto nyingi mno kiasi kwamba haiwezi kumudu anasa ya viongozi wake kutumia muda wa kazi kupanga safu, kuchimbiana mashimo na kupigana vita vya urithi wa madaraka.

Wananchi wanahitaji maji, barabara, ajira, huduma bora za afya, elimu yenye tija, masoko ya mazao na uongozi unaosikiliza. Hayo ndiyo yanayopaswa kuwa ajenda ya leo, siyo mbio za kesho kwenda Ikulu.

Pambazuko tunaamini hakuna mkulima kutoka kijijini aliyeunda kundi la kuandaa rais wa mwaka 2030. Hakuna mama lishe anayekaa usiku kucha kupanga mrithi wa urais. Hakuna kijana asiye na ajira anayehangaika na kambi za madaraka. Wenye makundi haya ya kusaka urais ni hawa viongozi wetu, ambao walipaswa kuwa kazini kuwatumikia Watanzania.

Ndiyo maana tunasema kwa uwazi, waache. Wafanye kazi. Wamtumikie Mtanzania wa leo kabla hawajaanza kugombania Tanzania ya kesho.

Waelewe kuwa urais siyo mali ya makundi; ni dhamana ya wananchi na yeyote anayejenga njia yake ya Ikulu kwa kumchafua mwenzake, anatuonyesha mapema kwamba huenda hana ukubwa wa kuaminika na taifa, kiasi cha kuachwa aendelee na mipango ya kuingia Ikulu zetu za Dodoma na Magogoni, Dar es Salaam.

Ikiwa kutakuwa na kulelewa kwa makundi haya na "wakubwa," sisi Pambazuko kutasimama na kuwakataa mbele za umma.

Tujenge Tanzania sasa. Tuache makundi ya kuchafuana yanayotumia muda kutangaza wingi wa boriti kwenye macho ya wenzao wakati wao macho yao yamejaa vibanzi.

# Ukarabati bado tu...




*Kamera ya Pambazuko imekuta Kituo cha Mabasi ya Mwendokasi (Udart) Manzese, Dar es Salaam hakijafanyiwa matengenezo yoyote hadi juzi – Jumamosi, ikiwa ni takribani miezi nane sasa tangu Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba aagize kukarabatiwa haraka kwa miundombinu katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya iliyoharibiwa kwenye vurugu wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka jana- 2025. (Na Mpigapicha Wetu)*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |


***Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz***

# Dunia: Hapa na Pale

## Wakosa Kombe la Dunia

WAANDISHI kadhaa wa habari kutoka Afrika na Iran wameripotiwa kunyimwa viza za kuingia Marekani kwa ajili ya kuripoti fainali za Kombe la Dunia 2026, hatua iliyozua wasiwasi kuhusu uhuru wa vyombo vya habari katika mashindano hayo.

Chama cha Kimataifa cha Waandishi wa Habari za Michezo, AIPS, kimeiomba Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) kuingilia kati kuhakikisha waandishi waliopata ithibati rasmi hawazuiliwi kutekeleza majukumu yao.

Kwa mujibu wa AIPS, baadhi ya waandishi wamekumbana na vikwazo vya viza, huku wengine wakipewa vibali vyenye masharti yanayoweza kuathiri kazi yao ya kufuatilia timu na matukio mbalimbali.

Hatua hiyo imeibua mjadala kuhusu wajibu wa nchi mwenyeji kuhakikisha usawa na mazingira huru kwa wanahabari wote.

## Taka Sifuri silaha tabia nchi

MKE wa Rais wa Uturuki, Emine Erdoğan, amesema harakati za "Taka Sifuri" zinapaswa kutazamwa kama nguzo muhimu katika juhudi za dunia kuhimili mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumza katika Jukwaa la Kimataifa la Taka Sifuri mjini Istanbul, Erdoğan alisema tatizo la taka siyo suala la usafi pekee, bali linagusa matumizi mabaya ya rasilimali, uchafuzi wa mazingira na mustakabali wa vizazi vijavyo.

Alisisitiza kuwa kupunguza taka, kuchakata bidhaa na kubadili tabia ya matumizi kunaweza kusaidia kupunguza athari za ongezeko la joto duniani.

Erdoğan amesema dunia inahitaji mshikamano wa pamoja ili kujenga uchumi endelevu, miji safi na mazingira salama kwa binadamu na viumbe wengine.



## Ebola yakwamisha biashara

WAFANYABIASHARA katika mpaka wa Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wameeleza kupata hasara kubwa kufuatia hofu ya kusambaa kwa ugonjwa wa Ebola.

Baadhi ya wafanyabiashara wamesema idadi ya wateja imepungua kwa kiasi kikubwa baada ya mamlaka kuimarisha ukaguzi wa afya na wananchi wengi kuogopa safari zisizo za lazima.

Bidhaa zinazoharibika haraka kama vyakula, matunda na mbogamboga zimeathirika zaidi, huku wasafirishaji wakilalamikia kuchelewa kwa mizigo.

Wadau wa biashara wameiomba serikali kuongeza kasi ya utoaji elimu ya afya, vifaa vya kujikinga na uratibu wa mipakani ili kudhibiti ugonjwa bila kuua uchumi wa wananchi wanaotegemea biashara ndogo ndogo.



## Shambulio la papa laua

MWANAMUME mmoja amefariki dunia baada ya kushambuliwa na papa katika pwani ya Australia Magharibi, tukio lililotokea karibu na kisiwa cha Michaelmas, eneo la Albany.

Kwa mujibu wa taarifa za polisi, kijana huyo mwenye umri wa miaka 35 alikuwa akivua samaki kwa kutumia mkuki akiwa na familia yake kabla ya kushambuliwa na papa anayekadiriwa kuwa na urefu wa mita 4.5.

Waokoaji na wahudumu wa afya walifika eneo la tukio baada ya taarifa kutolewa, lakini jitihada za kuokoa maisha yake hazikufanikiwa.

Tukio hilo limeibua hofu kwa wakazi na watalii wanaotembelea maeneo ya bahari, huku mamlaka zikitoa mwito wa tahadhari na kuripoti mara moja uwepo wa papa baharini.

Na Mzee TAI

# Waafrika Kusini waache ujinga




KUNA mambo yakitokea Afrika, mtu unabaki unacheka kwa uchungu. Unajiuliza; hivi sisi Waafrika tulikosea wapi? Au kuna mtu alituroga akili tukasahau historia yetu, damu yetu na madeni yetu ya kindugu?

Leo, baadhi ya raia wa Afrika Kusini wanawafukuza Waafrika wenzao kwa madai kwamba wamechukua kazi zao, wamebana fursa zao na kuifanya nchi yao kuwa ngumu kuishi. Ajabu iliyoje!

Sasa hawa wanaamini kuwa tatizo la ukosefu wa ajira Afrika Kusini siyo mfumo wa uchumi, siyo siasa za ubaguzi zilizorithiwa, siyo rushwa, siyo sera mbovu, siyo pengo la kipato, bali ni Mmalawi anayeuza nyanya, Mzimbabwe anayefanya kazi ya ulinzi, Msumbiji anayepaka rangi nyumba, au Mtanzania anayejitafutia mkate wake kwa jasho?

Huu ni ujinga uliovaa koti la uzalendo. Ni umasikini wa fikra unaojifanya kulinda taifa. Ni aina ya upofu unaomfanya mtu ampige jirani yake maskini, huku akimuachia tajiri aliyemnyonya kizazi hadi kizazi akiendelea kunywa kahawa kwenye kivuli cha utajiri.

Hawa raia wa Afrika Kusini wanaosahau historia, kwamba waliowaokoa kutoka kwenye uonevu wa makaburu ni damu na jasho la ndugu zao hao wanaowafukuza. Afrika Kusini haikujikomboa peke yake. Uhuru wake haukushuka kutoka mawinguni kama mvua ya neema. Ulitengenezwa kwa machozi, damu, jasho na sadaka za mataifa jirani. Tanzania, Zambia, Msumbiji, Angola, Zimbabwe na wengine walibeba mzigo wa mapambano dhidi ya makaburu.

Hivi vichwa vyao sijui vikoje, yaani wanajitoa ufahamu wakisahau kuwa walitoa ardhi, hifadhi, mafunzo, diplomasia na hata maisha ya watu wao ili ndugu zao wa Afrika Kusini waone jua la uhuru, ni hao wanaowafurusha leo.

Leo, wajukuu wa waliolindwa wanawafukuza wajukuu wa waliowalinda. Hapo ndipo Afrika inapochekesha na kuliza kwa wakati mmoja.

Kibaya zaidi, siyo raia wa kawaida pekee wanaobeba chuki hii dhidi ya wenzao waliookoa hata uhai wao. Wapo pia baadhi ya wenye mamlaka wanaoitazama sumu hii kama mtaji wa kisiasa. Badala ya kuelimisha jamii, wao wanacheza ngoma ya hasira za wananchi.

"Wakubwa hawa wanajua kabisa wahamiaji siyo chanzo kikuu cha matatizo ya Afrika Kusini, lakini ni rahisi kumlaumu mgeni kuliko kukiri kushindwa kwa uongozi.

Afrika Kusini inapaswa kuwa darasa la mshikamano wa Kiafrika, siyo uwanja wa aibu. Taifa lililopata uhuru kwa nguvu ya umajumui wa Afrika, halipaswi kuwa kinara wa kumdhalilisha Mwafrika mwenzake.

Swali linabaki; nani ametuнего? Au tumekubali wenyewe kuwa wajinga wa historia yetu na kusahau wote waliosaidia kukomeshwa kwa ubaguzi wa rangi na maisha huko Bondeni – almaarufu kwa Madiba?

Maana Mwafrika anayemfukuza Mwafrika mwenzake kwa sababu ya njaa, wakati wote wawili ni wahanga kukomesha mfumo uleule wa unyonyaji, siyo mzalendo. Ni mgonjwa anayempiga mgonjwa mwenzake wodini, akidhani ndiye daktari aliyemnyima dawa.

Pamoja na kutokubaliana na siasa za mmoja wa vijana machachari wa Afrika Kusini aitwaye Julius Malema, sasa akiwa kiongozi wa chama cha EFF, lakini katika kukemea ujinga wa kufukuza Waafrika wenzao huko Bondeni, naungana naye.

# Mwanga, giza bajeti mpya



*Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar*

Na Peter NYANJE

WATANZANIA wanasubiri kusikia mbivu na mbichi katika Bejeti Kuu ya Serikali itakayosomwa bungeni Alhamisi wiki hii - Juni 11.

Matarajio ya wengi ni kuona endapo bajeti hiyo italeta afueni kwa maisha ya sasa ambayo yametingwa na mazonge mengi magumu, ikiwamo kupanda kwa bei ya mafuta.

Lakini hilo linaweza lisionekane zaidi kwani uchambuzi uliofanywa na Pambazuko umebaini kuwa serikali yenyewe inakabiliwa na wakati mgumu katika utekelezaji wa bajeti ijayo kutokana na sababu kadhaa, kubwa ikiwa ni hatua ya wafadhili wengi kuamua kupunguza, kusitisha au kutishia kufuta kabisa misaada kwa Tanzania.

Kwa miaka kadhaa sasa, kwa wastani Bajeti ya Tanzania inategemea misaada na mikopo kwa ajili ya kujazia mfuko mkuu unaotoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni utegemezi huo umekuwa ukipungua kutoka wastani wa asilimia 30 hadi 11 katika bajeti ya mwaka 2024/25.

Kwa maana hiyo, hatua ya wafadhili kupunguza au kufuta misaada na mikopo itaathiri kwa kiasi kikubwa mipango ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ijayo.

Hii inamaanisha kuwa serikali italazimika kutafuta fedha nyingi zaidi kutoka vyanzo vya ndani ili kuziba pengo hilo, jambo litakaloathiri masoko ya fedha ya ndani ya nchi, hasa kwa wakopaji wadogo wadogo.

### Mizigo iliyopita

Lakini kikwazo kingine kikubwa katika utekelezaji wa bajeti ijayo kinatokana na utamaduni ambao umejengeka kwa miaka kadhaa sasa katika mifumo ya utekelezaji wa bajeti za kila mwaka.

Kwa kawaida kila wizara huenda bungeni kuomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali kwa upande wa maendeleo na pia fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Hata hivyo, imekuwa kama desturi sasa kuwa licha ya kuidhinishiwa na bunge, fedha hizo hakuna mwaka ambapo zimewahi kutolewa zote.

Uchambuzi uliofanywa na Pambazuko kwa kupitia ripoti za utekelezaji wa bajeti kwa miaka ya fedha mitatu iliyopita inaonyesha kuwa kwa wastani wizara nyingi, hasa zile zenye bajeti kubwa hupokea kati ya asilimia 80 na 85 ya fedha ilizoomba kwenye bajeti kwa mwaka.

Katika uchambuzi huo, Pambazuko limebaini kuwa katika 2024/25, Wizara ya Uchukuzi, ambayo ndiyo ilipata kiasi kikubwa cha fedha kuliko wizara nyingine yoyote, ilitengewa shilingi trilioni 2.72, lakini hadi mwisho wa mwaka huo, fedha zilizopokelewa na wizara hiyo zilikuwa ni asilimia 85 tu ya bajeti iliyoombwa.

Hali ni kama hiyo kwa Wizara ya Nishati ambayo ilitengewa kiasi cha shilingi trilioni 1.88, lakini hadi mwaka unaisha ikaishia kupe-

Inaendelea Uk. 7

# Mwanga, giza...

Inatoka Uk. 6

wa asilimia 85 tu ya fedha zilizokuwa zimetengwa.

Wizara ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha shilingi trilioni 1.76, lakini ikaishia kupewa asilimia 90 ya bajeti hiyo huku Wizara ya Afya ikipatiwa asilimia 85 ya bajeti ya shilingi trilioni 1.31 zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge.

Kwa upande wake, Tamisemi iliomba na kuidhinishiwa bajeti ya shilingi trilioni 1.1 lakini hadi mwaka unakamilika ilikuwa imepatiwa asilimia 90 tu ya bejeti hiyo.

Kabla ya hapo, mwaka 2023/24, Wizara ya Uchukuzi ilikuwa imetengewa shilingi trilioni 2.4, lakini hesabu zinaonyesha kuwa hadi mwisho wa mwaka huo ilikuwa imepokea asilimia 80 tu ya fedha hizo.

Katika mwaka huo, Wizara ya Nishati ilitengewa kiasi cha shilingi trilioni 1.9, lakini ikaambulia kupewa asilimia 80 tu ya bajeti hiyo wakati Wizara ya Ujenzi ikipokea asilimia 85 tu ya bajeti ya shilingi trilioni 1.5 ambazo zilikuwa zimeidhinishwa na Bunge.

Hali hii inamaanisha kuwa wakati serikali inapoingia katika mwaka mwingine wa fedha inakuwa imebeba viporo vya utekelezaji wa bajeti iliyopita.

Katika kufuatilia uwasilishaji, mjadala na upitishaji wa bajeti imebainika kuwa katika bajeti ya kila mwaka, masuala kuhusu fedha ambazo zilitengwa kwa wizara kwa mwaka uliopita - lakini hazikutolewa, halijadiliwi kwa kina na kuzingatiwa.

Matokeo yake, kila mwaka serikali inajikuta ikiwa na miradi kadhaa yenye thamani ya matrilioni ya shilingi ambayo utekelezaji wake haukufanikiwa kutokana na kutopatiwa fedha.

Lakini inapokuja bajeti mpya, mingi ya miradi hiyo haihesabiwi tena katika bajeti hiyo, lakini kwa kuwa serikali ilishaiwasilisha bungeni, basi baadhi ya wabunge huendelea kuipigia kelele kuitaka serikali itekeleze.

Hivyo, mara kadhaa serikali hulazimika kutoa fedha kutoka katika bajeti ya mwaka husika ili kutekeleza miradi iliyokuwemo kwenye bajeti zilizopita hata kama miradi hiyo haikutengewa fedha katika mwaka huo.



Mfano mzuri ni madeni ya wakandarasi na watoa huduma serikalini.

Pambazuko imebaini kuwa kila mwaka serikali hujikuta ikilazimika kutoa fedha kutoka kwenye bajeti iliyotengwa kwa ajili ya miradi mingine ili kulipa madeni hayo ambayo yanatokana na kutolipwa katika bajeti zilizopita kwa sababu licha ya kutengewa fedha lakini fedha hizo hazikutolewa.

Kwa ujumla, Pambazuko limebaini kupitia taarifa kutoka Wizara ya Fedha na vyanzo vingine kuwa kwa mwaka 2023/24 serikali iliidhinisha bajeti ya takribani shilingi trilioni 44.39, lakini hadi kufikia Aprili 2024, yaani miezi miwili kabla mwaka huo ufikie mwisho, ilikuwa imekusanya na kupata takribani shilingi 35.25 trilioni, sawa na asilimia 79.4 ya lengo la mwaka.

Hii ina maana kulikuwa na upungufu wa takribani shilingi trilioni 9.14 dhidi ya makadirio ya awali na katika wizara zilizoathirika sana ni zile zinazotengewa kiasi kikubwa cha bajeti ambazo ni Uchukuzi, Nishati, Ujenzi, Afya na Tamisemi.

Inaendelea Uk. 8




# Mwanga, giza...

Inatoka Uk. 7

**Makusanyo ya ndani**

Lakini wakati wizara zikikosa migawo ya bajeti zao takwimu za Wizara ya Fedha zinaonesha kuwa katika miaka ya hivi karibuni serikali kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA), imekuwa ikivuka lengo la makusanyo ya ndani kila mwaka.

Mathalan, katika mwaka 2023/24, kwa mara ya kwanza makusanyo ya ndani yalivuka lengo, jambo linaloashiria kuimarika kwa usimamizi wa kodi, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kuimarika kwa nidhamu ya ukusanyaji wa mapato.

Muhtasari wa ukusanyaji mapato unaonesha kuwa kwa mwaka huo serikali ililenga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 34.61 lakini ikafanikiwa kukusanya shilingi trilioni 34.85 ikiwa ni asilimia 100.7 ya malengo.

**Kwa nini fedha hazitoki zote**

Lakini mafanikio haya yanaacha swali kuwa kwa nini serikali inashindwa kuzipatia wizara kiasi cha fedha zinazoidhinishwa na Bunge kila mwaka wakati makusanyo yanaongezeka?

Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali, Hazina inashindwa kutoa fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa kutokana na pengo linalotokana na kutotekelezwa kwa ahadi za fedha kutoka kwa wafadhili.

Uchambuzi wa Pambazuko umebainisha mathalan kuwa kwa mwaka 2024/25 serikali ilikuwa imepanga kupata shilingi trilioni 5.55 kutoka kwa wafadhili kupitia misaada na mikopo lakini hadi mwisho wa mwaka zilipatikana shilingi trilioni 3.89 na kuacha pengo la shilingi trilioni 1.66.

Kwa maneno mengine, katika mwaka huo Tanzania ilipokea takribani asilimia 70 ya fedha zote za nje zilizokuwa zimepangwa kwenye bajeti ya 2024/25, huku upungufu mkubwa ukitokana na kuchelewa au kutokutolewa kwa baadhi ya mikopo ya maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo. Ripoti ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/23 inaonesha kuwa wafadhili walitoa shilingi bilioni 596 tu kati ya shilingi trilioni 1.1 za misaada zilizoahidiwa.

Kutokana na hali hiyo, serikali ililazimika kufidia pengo hilo kwa kuongeza ukopaji wa ndani hadi kufikia shilingi trilioni 4.61, zaidi ya mara 1.8 ya lengo la awali la shilingi trilioni 2.48 kwa mikopo mipya ya ndani.

**Hali itakuwaje mwakani?**

Wachambuzi wa masuala ya uchumi wanasema hali ya upatikanaji wa fedha itakuwa mbaya zaidi katika mwaka ujao wa fedha kutokana na wafadhili wengi kuonyesha dhamira ya kupunguza au kusitisha misaada kwa Tanzania kutokana na vurugu za Uchaguzi Mkuu mwaka jana - 2025.

Bunge la Ulaya lipo katika mchakato wa kupitisha azimio la kusitisha misaada ya mabilioni ya shilingi kwa Tanzania wakati Seneti ya Marekani nayo ipo katika mchakato wa kutunga sheria ya kuiwekea Tanzania vikwazo.

Wachambuzi wanasema katika hali kama hiyo serikali italazimika kuchukua hatua zilezile za kukopa fedha zaidi za ndani na hilo tayari lilishabainishwa na Waziri wa Fedha, Hamis Mussa Omar, wakati akiwasilisha ukomo na mwelekeo wa bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Kwa mujibu wa wachambuzi, hatua hiyo ya kuongeza kukopa ndani ina faida na hasara zake.

Inaendelea Uk. 9

# Mwanga, giza...

Inatoka Uk. 8

Kwa upande wa faida, wanasema kwanza serikali itakuwa inajijengea uwezo wa kugharamia bajeti yake bila kutegemea wafadhili.

Faida nyingine inatajwa kuwa serikali itakuwa na uhakika wa kuzipata fedha hizo na haitakuwa bahati nasibu kama ilivyo kwa fedha za wafadhili.

Faida nyingine inatajwa na wachambuzi kuwa ni manufaa watakayoyapata wawekezaji wa ndani katika mifuko ya uwekezaji.

"Kwa kuwa serikali itakopa zaidi ndani ina maana kuwa mifuko hii itakuwa moja ya vyanzo vikubwa vya fedha kwa serikali hivyo wawekezaji wake watanufaika sana," anasema mhadhiri mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam bila kupenda kutajwa jina lake.

Lakini, kwa upande mwingine, uamuzi huu wa serikali kukopa ndani utawaumiza wakopaji wengine ndani ya nchi.

Wachambuzi wanasema taasisi nyingi za fedha zitapenda kuikopesha serikali kutokana na hatari ndogo iliyopo na hivyo kupunguza mikopo yake kwa watu binafsi na taasisi zinazochipukia, jambo ambalo linaweza kupunguza shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wafanyabishara wadogo ambao ni muhimu katika kujenga uchumi binafsi na wa ngazi ya kati.

**Bajeti yenyewe**

Kwa mujibu wa mapendekezo yaliyowasilishwa na Waziri wa Fedha mwezi Machi mwaka huu, serikali inapanga kukusanya na kutumia shilingi trilioni 62.33 katika mwaka ujao wa fedha, likiwa ni ongezeko la asilimia 10.3 ukilinganisha na bajeti ya sasa ya shilingi trilioni 56.49.

Moja ya maeneo makubwa yanayopewa kipaumbele katika bajeti ya 2026/27 kwa mujibu wa Waziri Omar ni uwekezaji katika miradi ya maendeleo, hasa katika sekta za miundombinu, nishati, maji, afya na elimu.

Waziri wa Fedha alisema uwekezaji huo ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha huduma kwa wananchi na pia kuendeleza miradi ambayo tayari ilishaanzishwa.

"Serikali itaendelea kuwekeza katika miradi ya kimkakati ya maendeleo ambayo inalenga kuimarisha miundombinu, kuongeza tija ya uzalishaji na kuchochea ukuaji wa uchumi," alisema.

Hadi hivi sasa uwekezaji katika miundombinu umechangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi katika miaka ya hivi karibuni, ingawa baadhi ya miradi bado haijakamilika.

Jambo jingine lililojitokeza katika bajeti hiyo ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza Julai Mosi mwaka huu ni mkazo mkubwa uliowekwa katika kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwa lengo la kupunguza utegemezi wa misaada na mikopo kutoka nje.

Hilo lilitarajiwa na watu wengi hasa baada ya misaada kutoka nje kuanza kupungua kutokana na kashfa ya vurugu za kisiasa zilizoandamana na uchaguzi mkuu uliopita, ambazo zimeharibu taswira ya nchi nje.

Ili kulifanikisha hilo, Waziri wa Fedha anasema serikali itajikita katika kupanua wigo wa walipa kodi na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kutumia teknolojia za kidigiti ili kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa wingi.

"Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kupanua wigo wa walipa kodi, kuimarisha usimamizi wa kodi na kutumia mifumo ya kisasa ya kidigitali," alisema.

**Kilimo, uzalisha, viwanda**

Aidha, bajeti ya 2026/27 inaendelea kusisitiza maendeleo ya sekta za uzalishaji kama kilimo, viwanda, madini na utalii, ambazo zinaonekana kuwa nguzo muhimu za uchumi wa Tanzania.

Serikali inaamini kuwa kuimarisha sekta hizo kutasaidia kuongeza ajira, kuongeza uzalishaji na kukuza mauzo ya nje.

Waziri wa Fedha alisema serikali itaendelea kuwekeza katika sekta hizo ili kuongeza thamani ya bidhaa za ndani na kukuza ushindani wa Tanzania katika masoko ya kimataifa.

"Lengo letu ni kuimarisha sekta za uzalishaji ili ziweze kuongeza thamani ya bidhaa za ndani, kukuza ajira na kuongeza mapato ya taifa," alisema.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Yuda amechokozwa, vyema asichokozeke

YUDA wa Biblia alimsaliti Bwana Yesu. Siamini kama mleta hoja anamaanisha msalitiwa katika hoja yake ni sawa na Bwana Yesu! Ipo siku tusiyoijua, "Yesu" huyu aliyefumbwa katika hoja hii, atafananishwa na "Mtume" asiyelinganishwa. Hapatatosha. Mleta hoja hajachagua vizuri maneno yake na mifano yake. Nimemsamehe bure.

Sakata hili lina mapichapicha ya hatari. Hapa nayafafanua.

Msemaji aliwahi kuchokonoana na rais wake huko kwao mpaka akaachia ngazi. Mama yetu akamchukua, akamteua. Ina maana rais yule na mama yetu hawako pamoja na hawaivi? Je, mama ni Yuda wa rais yule kwa kuwa alimchukua mleta hoja ambaye ni msaliti wa rais yule?

Mleta hoja ni Mzanzibari, anamnanga Yuda Mtanganyika. Hii ni kero au ufa katika muungano? Alikosekana Mtanganyika wa kumrudi Yuda Mtanganyika?

Mleta hoja anasali Ijumaa; anamnanga anayesali Jumapili kwa kutumia picha ya (Yuda) anayeomba huruma makanisani. Tuseme katumwa na msikiti?!

Maneno yake yameingia kwenye Hansard. Bunge halikukanusha. Je, ni bunge zima linamwita makamu kuwa ni Yuda?

Naibu Spika alipomwongoza ajikite kwenye hoja, wabunge walipiga makofi. Walifurahia kiongozi wao kuingilia au walimshangilia mtoa hoja. Je, makofi hayo ni mashangilio ya tumbili wa Kijaluo anayeshangilia pori linaloungua bila kuwaza atalala wapi usiku?

Hoja imetolewa siku rais ameondoka nchini na kwa mujibu wa katiba, makamu ndiye mkuu wa nchi wa zamu. Mtoa hoja anamaanisha hamtambui makamu kuwa mkuu wa nchi wa zamu?

Kwa vyovyote, kuna dalili mbaya. Matiti ya binti wa Kijaluo yakiishaota, hayafichiki na hayarudi nyuma.

Wakristo wanaamini usaliti wa Yuda ulileta wokovu. Bila usaliti, Yesu asingekufa. Bila kifo, asingefufuka; na bila kufufuka, wokovu usingepatikana. Hakuna wokovu bila usaliti.

Waliookoka wameisaliti dhambi ili wawe huru. Mleta hoja kakosea. Hakuna Yuda na hakuna Yesu katika hoja yake. Zilikuwa ni saa za jioni; Dodoma mapito ni mengi, hatujui alipitia wapi kuja bungeni.

Kisiasa, CCM bila tishio la upinzani wa nje, inayumba. Tulishauri mapema sana Tundu Lissu aachiwe ili aiunganishe CCM, tukapuuzwa.

Angeachiwa mapema, CCM ingeungana na kusahau tofauti zake za ndani ili kukabiliana na upinzani. Hivi sasa wapo wana CCM wanamtamani Lissu ili awasaidie kuona thamani ya umoja wa chama chao. Hawajachelewa.

Mama alikuja na "R" nne. Moja ya "R" hizo ni Reforms, yaani mabadiliko. Lissu akamuunga mkono mama kwa kusema "Bila Mabadiliko, Hakuna Uchaguzi" (No refors, No election). Akakamatwa kwa uhaini wakati aliunga mkono falsafa ya 4R! Mbadilishie mashtaka mseme alikosea kumuunga mkono mama!

Wenye madaraka punguzeni nguvu, ongezeni hekima. William Ruto alipata urais kwa huruma ya kudhaniwa anaonewa na Uhuru Kenyata. Akakosea, akatumia nguvu kumwondoa makamu wake Rigathi Gachagwa. Hivi sasa ana nguvu binafsi, lakini urais (presidency) ni dhaifu.

Kambarage alitumia nguvu na hasira Januari 30, 1984. Mpaka anaondoka duniani, jambo hilo lilimtesa. Donald Trump alimnanga makamu wake Mike Pence hadharani, akaangushwa na Joe Biden kwenye uchaguzi. Rais na makamu wake hawatenganishwi kirahisi. Siyo mnatuimbia maridhiano!? Ridhianeni basi ili machawa tukose kazi.

Kama Yuda alichokoza; aliyechokozwa asichokozeke. Kama Yuda amechokozwa; asichokozeke.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

## Kona ya Dkt. Bisimba

# Kipi ni kipimo cha usalama wa raia

SIKU za hivi karibuni katika ziara anazofanya Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba lipo tukio ambalo linaleta mawazo mazito kuhusu usalama wa raia.

Tukio hilo linaweza kutafsiriwa kuwa siyo suala la mtu mmoja aliyepata fursa kufika mbele ya waziri mkuu, bali ni hali inayogusa jamii nzima kuhusu usalama wao.

Katika tukio husika yuko mama mmoja alieyeelezea jinsi watu waliofika nyumbani kwake na kujitambulisha kuwa ni askari polisi na kisha kumchukua kijana wake wa miaka 32.

Watu hao walipoulizwa wanampeleka wapi kijana huyo na ana kosa gani, hawakuwa na jibu zaidi ya kuwataka ndugu hao kurudi ndani.

Kijana alifungwa pingu akaingizwa kwenye gari pakiwepo na askari mwenye silaha. Mama huyo anaeleza walikwenda Kituo cha Polisi wakaambiwa kijana wao hajafikishwa hapo, wakaambiwa uchunguzi utafanyika.

Lakini siku mama huyo akiongea na waziri mkuu ilikuwa ni siku ya arobaini wakiwa hawajamuona kijana wao na hawajapata majibu yoyote kutoka polisi kuhusu alipo kijana huyo au hatma yake.

Tukiangalia kisa hiki kinaibua masuala kadhaa ya kiusalama na haki tulizo nazo kama raia wa nchi hii.

Kwanza, tufahamu kuwa usalama wa raia haupimwi tu kwa kutokuwepo kwa uhalifu, bali utapimwa kwa uhakika kwamba mtu anaposhikiliwa na mamlaka, familia yake ijulishwe alipo na pia sababu ya mtu huyo kushikiliwa.

Pili, utawala wa sheria unahitaji uwazi. Anapokamatwa mtu kwa sababu zinazokubalika kisheria lazima pawepo na kumbukumbu za kukamatwa kwake na alipowekwa na pia taarifa za kufikishwa mahakamani kwa muda unaokubalika kisheria.

Hali ya mtu kuchukuliwa na kisha asionekane bila taarifa ni kuzua hofu kwa jamii.

Taasisi za serikali katika hili zinapaswa kutoa majibu kwa kufanya uchunguzi iwapo si zenyewe zinazohusika na upoteaji huo.

Hapa lazima tukumbuke kuwa usalama ni sehemu ya haki za binadamu. Ninapoongea kuhusu kisa hiki kimoja ambacho sasa kinaanza kuwa kama utamaduni hapa nchini, ninaangalia iwapo kweli wananchi tunaweza kuwa na imani na mifumo ya usalama nchini.



*Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba*

Watu huwa na imani na polisi na ndiyo maana mara zote pakitokea jambo hukimbilia polisi. Polisi wanapokosa majibu ya kuridhisha na huku inasemekana aliyechukuliwa na polisi inaleta taswira mbaya sana kwamba kuna hali ambazo zinaweza kutokea bila polisi kufahamu.

Kwa hapa tulipofikia kama nchi tukisikiliza kilio cha huyu mama mbele ya waziri mkuu kinaweza kuwa kinaakisi mambo makubwa zaidi kuhusu uhusiano uliopo kati ya wananchi na taasisi za umma ikiwamo Jeshi la Polisi.

Tunaiona sauti ya hofu, isiyo na matumaini na hakuna pa kuyapeleka. Ni kama vipo vilio vya wengine wengi ambao hawajapata majibu, hapa raia tufanye nini? Kipimo cha usalama wetu kama raia ni uwezo wa vyombo husika kulinda haki na kuwa na majibu ya watu wanaopotea.

Je, wananchi wakikosa imani kutokana na matukio haya, nchi itaweza kuwa salama. Je, ni kila mtu anaweza kumfikia waziri mkuu?

Inatakiwa taasisi husika iweze kusikiliza na kutatua matatizo ya raia katika ngazi yake. Hali hii inazua suala la uhusiano kati ya raia na dola kuingia doa.

Tukio hili tulitazame kwa macho ya kutafuta mabadiliko makubwa ya mifumo ya utawala na usalama nchini. Tunapaswa kuishi bila hofu.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Habari

# Nini kitarajiwe ziara ya Samia Russia




*Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Russia, Vladmir Putin katika Kongamano la Kimataifa la Uchumi la St. Petersburg (SPIEF'26).*

**Na Mwandishi WETU**

NI wazi kwamba ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Russia, inalenga kukuza uhusiano wa kihistoria uliopo kati ya Tanzania na nchi hiyo kwa kufungua fursa mpya za kiuchumi kwa nchi hizo mbili.

Ziara hiyo ambayo ni ya kwanza kwa Rais Samia nje ya Afrika tangu vurugu za Oktoba 29,2025, pia ni ya pili kufanywa na Rais wa Tanzania nchini Russia (Wakai huo ikiitwa Urusi) tangu mwaka 1969 alipozuru Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Rais Samia amefanya mazungumzo na Rais wa Russia, Vladimir Putin mjini Moscow huku viongozi wote hao wakieleza kuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha uhusiano wa kihistoria kati ya nchi hizo.

Katika mazungumzo yaliyofanyika ndani ya Ikulu ya Kremlin, Putin alimkaribisha Rais Samia na kueleza kuridhishwa kwake na mwenendo wa uhusiano kati ya nchi zao huku akikumbusha kuwa mwaka huu Tanzania na Russia zinatimiza miaka 65 tangu kuanzishwa kwa uhusiano wa kidiplomasia.

Rais Putin pia alieleza kuwa ni jambo la kipekee kwamba Rais Samia ameichagua Russia kuwa nchi ya kwanza ya kigeni kuifanya ziara rasmi ya kiserikali baada ya kuapishwa kwake.

"Biashara kati ya Russia na Tanzania imeendelea kukua kwa kasi, huku kiwango kikiongezeka kati ya asilimia 20 hadi 25 kwa mwaka 2025.

"Hatua hiyo inadhihirisha kuimarika kwa ushirikiano wa kiuchumi na kunufaisha wananchi wa Russia na Tanzania," amesema Rais Putin.

Katika mazungumzo hayo, Rais Putin aliweka bayana kwamba ukuaji huo wa uchumi unaonyesha kuimarika kwa ushirikiano wa kiuchumi na mahusiano ya kidiplomasia kati ya mataifa hayo mawili, yanayoadhimisha miaka 65 ya uhusiano wa kidiplomasia.

Akasema ongezeko hilo ni hatua muhimu na kusisitiza kuwa bado kuna fursa nyingi za kuongeza biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Urusi.

Inaendelea Uk. 13

# Nini kitarajiwe ziara ya Samia Russia

Inatoka Uk. 12

Alizitaja sekta za madini, usafiri na usafirishaji, afya na elimu kuwa miongoni mwa maeneo yenye nafasi kubwa ya kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi hizo mbili.

Kwa upande, Rais Samia amesema ziara hiyo itaimarisha ushirikiano na kukuza fursa za maendeleo kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na Russia.

Alisema pamoja na kujadili ushirikiano wa pande mbili, pia wamejadili namna ya kuendeleza maendeleo endelevu yatakayowanufaisha wananchi wa nchi zote mbili.

Rais huyo wa Tanzania pia aliishukuru Russia kwa mwaliko huo na kwa mchango wake katika historia ya bara la Afrika, hususan katika kipindi cha harakati za ukombozi wa mataifa mengi ya Afrika.

### Uwekezaji ajenda kuu

Miongoni mwa masuala yaliyopewa uzito mkubwa katika mazungumzo hayo ni kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi.

Putin amesema kuna fursa kubwa ya kuongeza biashara kati ya nchi hizo, ambayo kwa sasa inakadiriwa kufikia zaidi ya dola milioni 300 kwa mwaka.

Ingawa kiwango hicho bado ni kidogo ikilinganishwa na uwezo wa kiuchumi wa nchi hizo mbili, viongozi hao wameeleza nia ya kukiongeza kupitia ushirikiano katika sekta za madini, nishati, kilimo, utalii na usafirishaji.

Miradi inayotajwa mara kwa mara katika ushirikiano wa Tanzania na Russia ni mradi wa mgodi wa urani wa Mkuju, kusini mwa Tanzania.

Mradi huo umekuwa ukijadiliwa kwa zaidi ya muongo mmoja na unaonekana kuwa moja ya uwekezaji mkubwa wa Urusi nchini Tanzania.

Katika hatua nyingine ya kuimarisha uhusiano wa kiuchumi, Baraza la Biashara kati ya Russia na Tanzania liliundwa mapema mwaka huu.

Aidha, Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) tayari limetangaza mipango ya kuanzisha safari za moja kwa moja kati ya Dar es Salaam na Moscow kabla ya mwisho wa mwaka.



*Rais Samia akitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima (Honoris Causa) na Chuo Kikuu cha Urafiki wa Watu wa Urusi- (RUDN University) kutoka kwa mkuu wa chuo hicho, Profesa Oleg Yastrebov hafla iliyofanyika chuoni hapo Moscow wiki iliyopita.*

Rais Samia ameongozana na ujumbe wa wafanyabiashara na maofisa wa serikali, jambo linaloonyesha dhamira ya Tanzania kutumia ziara hiyo kuvutia uwekezaji mpya na kufungua masoko zaidi kwa bidhaa na huduma zake.

### Diplomasia ya Tanzania

Ziara hiyo imefanyika wakati Russia ikiendelea kuimarisha uhusiano wake na nchi za Afrika kufuatia mvutano wake na mataifa ya Magharibi tangu kuanza kwa vita vya Ukraine mwaka 2022.

Inaendelea Uk. 14

Habari



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha RUDN wakiwa na bendera za Tanzania wakati Rais Samia akitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima.



Rais Samia aweka shada la maua kwenye kaburi la askari asiyejulikana (Tomb of the Unknown Soldier) pembezoni mwa ukuta wa Ikulu ya Kremlin.

# Nini kitarajiwe...

Inatoka Uk. 13

Kwa upande wa Tanzania, ziara hiyo imevutia pia uangalizi wa jumuiya ya kimataifa kutokana na changamoto za kidiplomasia zilizojitokeza katika mahusiano na baadhi ya mataifa ya Magharibi.

Mataifa ya Magharibi na mashirika ya kutetea haki za binadamu, yamekuwa yakikosoa hatua mbalimbali zilizochukuliwa dhidi ya wapinzani na wanaharakati nchini Tanzania.

Marekani imesema inapitia upya baadhi ya vipengele vya uhusiano wake na Tanzania, huku ofisa mmoja wa polisi akiwekewa vikwazo kutokana na madai ya ukiukaji wa haki za binadamu.

**Wasemavyo wachambuzi**

Katika mazingira hayo, wachambuzi wanaona ziara ya Samia huko Russia kama sehemu ya mkakati mpana wa Tanzania wa kuendelea kushirikiana na washirika mbalimbali duniani bila kujifungamanisha na upande mmoja wa kisiasa au kiuchumi.

Mhadhiri wa Elimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa George Kahangwa anasema ziara hiyo ya Rais Samia ni ya mkakati na kwamba analazimika kutokana na mazingira ya sasa ya kisiasa na kiuchumi.

"Sasa tumefika wakati huu misimamo ya mataifa ya Magharibu dhidi ya Samia, si unaona Marekani wametengeneza muswada wa sheria, huku EU na mambo yaliyofanyika wanakusudia kusitisha misaada ya kifedha.

Profesa Kahangwa ambaye pia ni mchambuzi wa masuala siasa na diplomasia, anasema hatua hiyo ya Mataifa ya Magharibi kujivuta kwa sababu ya yaliyotokea Oktoba 29,2025 ni sababu mojawapo ya Samia kujenga uhusiano na mataifa mengine ya Mashariki.

"Kwa yanayoendelea kiitikadi Rais Samia amekuwa na matumaini na Mataifa ya Mashariki na matarajio yetu sasa atafika China na Korea," amesema Profesa Kahangwa.

Kwa upande wake mtafiti na mchambuzi wa masuala ya uchumi na jamii, Steven Mmbogo alianza kwa kuhoji iwapo Tanzania inaweza kuwa na uhusiano mzuri na Russia.

"Swali la msingi ni kama Russia inaweza kuchukua nafasi ya kisiasa, kiuchumi na kifedha ambayo kwa miongo mingi imejengwa na nchi za Magharibi, Marekani na Ulaya…"

"Kwa mtazamo huo, ziara ya Rais Samia inaweza kueleweka kama ujumbe kwamba Tanzania ina chaguo mbadala endapo uhusiano wake na Magharibi utaingia katika misukosuko kutokana na yaliyotokea Oktoba 29,2025,"amesema Mmbogo. Anasema Russia inaweza kuwa mshirika wa kisiasa, lakini bado haijathibitisha kuwa mshirika mkubwa wa maendeleo kwa Afrika kwa kiwango cha Marekani na Ulaya.

Anafafanua kuwa Russia hujikita zaidi katika maeneo ya kimkakati kuliko maendeleo ya kijamii na ndiyo maana Afrika nzima hakuna mahali ambapo nchi hiyo imetoa ufadhili kwa kiwango kikubwa.

# Jaji Ruhangisa ashangaa sheria batili kutokufutwa



Na Mwandishi WETU

JAJI mstaafu wa Mahakama ya Afrika ya Mashariki, Profesa John Ruhangisa, ameishangaa serikali kushindwa kuviondoa vifungu vya sheria vilivyobatilishwa na mahakama kwa nyakati tofauti kwa kukinzana na Katiba ya Tanzania.

Amesema nguvu ya sheria yoyote inatokana na Katiba, na endapo itakinzana, ni dhahiri sheria hiyo ni batili.

Katika mahojiano maalum na Wakili TV wiki iliyopita, Jaji Ruhangisa (pichani) amesema sheria zote zilizoamriwa na mahakama kukinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinapaswa kufutwa.

Ingawa hakutaja baadhi ya sheria au vifungu ambavyo vilibatilishwa ambavyo bado havijaondolewa kwenye vitabu vya sheria, anasisitiza kuwa endapo mahakama imepewa madaraka ya kubatilisha sheria au kitendo chochote kilichofanywa na kiongozi ambacho kimekiuka Katiba, hakuna mtu yeyote wa kupinga.

Ameeleza kuwa sheria yoyote ikitungwa huku ikipingana na Katiba, mahakama ina mamlaka ya kuibatilisha na kwamba kwa kawaida mahakama itafafanua sheria hiyo imekinzana na Katiba kwa kiwango gani.

Jaji Ruhangisa, ambaye amewahi kuwa Mahakama Kuu ya Tanzania kabla ya kuteuliwa kwenye Mahakama ya Afrika Mashariki, amesema ukimya wa serikali kutofuta baadhi ya vifungu vilivyobatilishwa unashangaza.

"Vifungu batili vinapaswa kuondolewa, iwapo mahakama imetamka kuwa ni batili," amesema.

Anasema Katiba ni mwongozo wa jamii ambayo imekubali kukaa pamoja na kufanya mambo yao kwa pamoja, hivyo lazima mwongozo huo uheshimiwe.

Na hakuna mtu aliye juu ya sheria na hata kiongozi anaapa kuilinda Katiba, sambamba na wananchi ambao pia wana wajibu wa kuheshimu viongozi pale ambapo wanasimamia vyema Katiba.

"Ndiyo maana katika Katiba pendekezwa iliyotokana na mapendekezo ya wananchi, askari hatakiwi kutekeleza amri ambayo siyo halali. Kuna uelewa mbaya, mtu kujiona yeye ni askari, kiongozi wake akitoa amri lazima aitekeleze…"

"Huo wajibu upo kwake, ajue je hii amri ni halali? Kama siyo halali, inayokupeleka kukinzana na Katiba, hiyo siyo halali. Kiongozi usijione kwamba mimi mkuu wa jeshi, au polisi kwa hiyo naweza nikaamuru kamata huyu mtu piga, kwa mujibu wa miongozo kupiga siyo halali, huo ndiyo umuhimu wa Katiba, inadhibiti mtu kufanya utakavyo…"anasema.

Kuhusu uwakilishi wa wananchi bungeni, jaji huyo anasema Katiba haiwezi kuandika kila kitu kwa sababu imetengenezwa na watu, lakini kwa Tanzania wananchi wanawatumia wabunge kwa niaba yao kutunga sheria zinazofafanua sheria mbalimbali, lakini sharti zisikinzane na matakwa ya Katiba.


### Sheria zilizobatilishwa

Ingawa Jaji Ruhangisa hakutaja sheria hizo zilizobatilishwa, lakini ufuatiliaji wa Pambazuko umebaini kuwa ndani ya miaka michache iliyopita, mahakama za Tanzania - hasa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani - zimetoa uamuzi muhimu uliobatilisha au kutangaza baadhi ya vifungu vya sheria kuwa vinakiuka Katiba.

Mapema mwaka huu, Mahakama Kuu ilieleza kuwa kifungu cha 194 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kuwa siyo cha kikatiba kwa kuwa kilikuwa kinatoa haki kwa upande wa mashitaka ambazo upande wa utetezi haukuwa nazo.

■ Habari

# Vita urais 2030 yakolea CCM



Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi



Simai Mohamed Said

**Na Mwandishi WETU**

KAULI ya Mbunge wa Tunguu kutoka Zanzibar, Simai Mohamed Said kwamba kuna Yuda ndani ya serikali, imeibua mjadala kwenye mitandao ya kijamii kwa siku kadhaa sasa.

Kauli hiyo ilizua maswali mengi kuliko majibu huku wengine wakihoji Yuda ni nani, kwanini mbunge huyo ameamua kuzungumza sasa na kwanini achague kusema bungeni badala ya vikao halali vya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwasilisha ujumbe huo?

Kadiri mjadala wa Yuda unavyozidi kushika kasi, swali kubwa zaidi likaibuka; je, Simai anazungumzia usaliti ndani ya CCM pekee, au amefungua pazia la mapambano ya urithi wa kisiasa kuelekea kinyang'anyiro cha kumpata rais mpya kwenye uchaguzi wa mwaka 2030?

Ingawa Simai hakumtaja kwa jina Yuda ni nani, lakini wafuatiliaji wa mambo ya siasa wanasema aliyelengwa na kada huyo ni Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kutokana na mazingira.

Pamoja na hayo, wengi wanahoji kuwa walitegemea Spika wa Bunge angetaka maelezo kutoka kwa Simai kumtaja Yuda kwa jina kwa sababu alilisemea bungeni ambapo kunahitajika kanuni na miongozo ya bunge.

Dkt. Nchimbi anatajwa kuwa mmoja wa viongozi wenye matamanio ya kuwania urais baada ya Rais Samia kumaliza muda wake, 2030. Hata hivyo, kiongozi huyo hajathibitisha wala kukanusha kuhusu suala hilo.

**Hoja ya Simai**

Akichangia mjadala wa Bajeti ya Wizara Fedha bungeni Juni 2,2026, Simai alitoa kauli hiyo nzito akidai kuna usaliti ndani ya CCM na serikali.

Simai ambaye aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali serikalini akiwemo Waziri wa Elimu na Mafunzo Zanzibar na baadaye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale kabla ya kujiuzulu mwaka 2024, akiwa bungeni juzi alisema; "Kosa la mama liko wapi? Kwa sababu ya kumwamini mtu kumbe ni Yuda."

Akaongeza tena kuwa; "Yuda huyu amesaliti ndugu zake, hata ile familia ambayo ilimlea kisiasa, hawataki kumuona huyu Yuda. Hata huko nyuma amewahi kutajwa ni mzigo, lakini leo mzigo huu tunao ndani ya serikali."

Kwa mujibu wa Simai, mtu anayemzungumzia ameathiri wafanyabiashara, watendaji wa serikali na hata baadhi ya wanasiasa ambao safari zao za kisiasa zimekatizwa naye huyo Yuda.

Simai akasema kuwa Yuda huyo kwa sasa ameibuka katika nyumba za ibada kutafuta huruma.

Akitoa neno kwenye maziko ya mama mzazi wa hayati John Magufuli, Suzana Magufuli wiki iliyopita Chato mkoani Geita, Dkt. Nchimbi alisimulia kisa chake na Rais Magufuli kuanzia mwaka 2015 alipoamua kupumzika masuala ya siasa.

Inaendelea Uk. 17

# Vita urais 2030...

Inatoka Uk. 16

Pamoja na mambo mengine, Dkt. Nchimbi aliwaambia waombolezaji hao kuwa Rais Magufuli alimwambia kuwa hataharibu ndoto yake. Hakufafanua kuhusu ndoto hiyo, lakini wengi wanaamini ni nafasi ya juu ya uongozi wa Tanzania – urais.

Katika simulizi za Yesu Kikristo, Yuda Iskariote anakumbukwa kwa jambo moja kuu; kumsaliti Yesu, licha ya kuwa mmoja wa wanafunzi wake aliowaamini.

Ndiyo maana jina "Yuda" katika mazingira mengi ya kisiasa hutumiwa kuashiria usaliti, kutokuwa mwaminifu au kugeuka dhidi ya waliokujenga.

Pamoja na kwamba Simai hakufafanua moja kwa moja kwanini aliamua kuzungumza kwa mafumbo na kejeli, wakati maelezo yake yalikuwa wazi kung'amua ni nani anamlenga na lengo lilikuwa nini.

Wakati mjadala huo ukiendelea, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kupitia ACT-Wazalendo, Addo Shaibu alitoa tafsiri yake ya kisiasa kuhusu kinachoendelea.

Addo alisema; "Ninawaomba wabunge wa CCM homa yenu ya siasa kuelekea 2030 isiharibu majadiliano ya bunge hili."

**Mbio za urais hazipoi**

Licha ya kwamba taratibu za kuanza mbio za kumrithi Rais Samia Suluhu Hassan bado hazijaanza rasmi na kuwa wazi, lakini imekuwa ni mazoea ya waansiasa kwamba kila baada ya uchaguzi, mchakato wa ngwe nyingine huanza haraka.

Ndiyo maana wanaotamani kuwa viongozi wa Tanzania, huchukua zaidi ya miaka 10 wakijipanga kuingia Ikulu.

Hilo linaifanya mijadala yoyote kuhusu urithi wa kisiasa ndani ya CCM kutazamwa kwa jicho la tahadhari, hata kama hakuna mchakato rasmi ulioanza.

Wiki chache kabla ya kauli ya Simai, Makamu Mwenyekiti wa CCM, Stephen Wassira, naye aligusia jambo linalofanana na hilo.

> **"Nimeambiwa wengine wanazungumza urais wa mwaka 2030, leo? Tumemaliza uchaguzi mwaka jana, sasa si tujenge kwanza nchi?"**

Alisema; "Nimeambiwa wengine wanazungumza urais wa mwaka 2030, leo? Tumemaliza uchaguzi mwaka jana, sasa si tujenge kwanza nchi?"

Kauli hiyo ilionekana kama onyo kwa wanachama au viongozi ambao tayari wanaanza kufikiria uchaguzi unaofuata wakati harufu na kumbukumbu ya uchaguzi wa 2025 bado haijapotea.

Kwa chama kilichozoea kuwa madarakani kwa miongo kadhaa, mijadala ya urithi wa uongozi huwa inaanza mapema zaidi kuliko inavyoonekana hadharani.

Kwa wengi ndani ya CCM, uchaguzi wa mwaka 2015 unabaki kuwa mfano mkubwa wa jinsi ushindani wa ndani unavyoweza kuwa mkali, lakini pia jinsi ushindani huo unavyoweza kutikisa siasa za chama na taifa kwa ujumla.

Katika kipindi hicho, makundi mbalimbali yalijitokeza waziwazi. waziri mkuu wa zamani, Edward Lowassa alikuwa miongoni mwa wanasiasa waliotajwa kuwa na ushawishi mkubwa kabla ya kuhamia upinzani baada ya kutopitishwa na CCM.

Kulikuwa pia na makundi yaliyomuunga mkono aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Bernard Membe, huku mengine yakimuunga mkono John Magufuli ambaye hatimaye alipitishwa na kushinda urais dhidi ya Lowassa aliyekuja kuhamia upinzani - Chadema.

Lowassa na Membe wote sasa ni marehemu.

Miongoni mwa matukio yaliyokumbukwa zaidi ni kauli ya Emmanuel Nchimbi, ambaye sasa ni makamu wa rais, aliposema yeye pamoja na wajumbe wenzake wa Kamati Kuu ya CCM wakati huo, Sophia Simba na Adam Kimbisa, hawakukubaliana na baadhi ya uamuzi wa Kamati Kuu ya chama, kwa kumuengua Lowassa kuwa mgombea wa chama hicho.

■ Makala

# Teknolojia mpya kuhifadhi mazao yahuisha matumaini




*Mkulima wa Kijiji cha Milamate Wilaya ya Nsimbo mkoani Katavi, Mariamu Simoni, akionesha mazao yake yaliyohifadhiwa katika mifuko ya tabaka, teknolojia inayosaidia kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kulinda ubora wake wakati wa uhifadhi.*

**Na Mwandishi WETU**

WAKATI Tanzania ikiendelea kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, changamoto ya upotevu wake baada ya mavuno, imeendelea kuwa moja ya vikwazo vikubwa vinavyowakabili wakulima wengi.

Licha ya kutumia muda, nguvu na rasilimali nyingi katika uzalishaji, sehemu kubwa ya mavuno hupotea kutokana na wadudu waharibifu, unyevunyevu, ukungu na mbinu duni za uhifadhi.

Hali hiyo imekuwa ikisababisha hasara kwa wakulima, kupunguza upatikanaji wa chakula na kuathiri kipato cha kaya zinazotegemea kilimo.

Lakini sasa matumaini mapya yanaanza kuonekana kupitia matumizi ya teknolojia ya mifuko ya tabaka (Hermetic Bags), ambayo imeanza kuleta mabadiliko katika namna wakulima wanavyohifadhi mazao yao baada ya mavuno.

Inaendelea Uk. 19

# Teknolojia mpya...

Inatoka Uk. 18

Teknolojia hiyo inahamasishwa kupitia Mradi wa Usimamizi wa Mazao Baada ya Mavuno kwa Wakulima Wadogo, unaotekelezwa kwa ushirikiano wa Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT), Helvetas Tanzania, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), pamoja na Chuo Kikuu cha Zurich cha Uswisi.

Kupitia mradi huo, wakulima katika maeneo mbalimbali nchini wanapatiwa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mifuko ya tabaka kama njia ya kupunguza upotevu wa mazao na kuimarisha usalama wa chakula.

Mifuko ya tabaka ni teknolojia ya kisasa inayotumika kuhifadhi mazao ya nafaka na mikunde kama mahindi, mpunga na maharage bila kutumia kemikali za kuhifadhia mazao.

Mifuko hiyo hutengenezwa kwa matabaka maalumu yasiyopitisha hewa wala unyevunyevu, hali inayozuia wadudu kuendelea kuishi au kuzaliana ndani ya mazao yaliyohifadhiwa.

Kwa mujibu wa wataalamu wa kilimo, teknolojia hiyo siyo tu inapunguza upotevu wa mazao, bali pia inalinda afya za walaji kwa kupunguza matumizi ya kemikali ambazo zimekuwa zikitumika kwa kiwango kikubwa kuhifadhi nafaka.

**Elimu yaongeza mwitikio**

Dalili za mafanikio ya teknolojia hiyo zinaanza kuonekana katika maeneo mbalimbali yanakotekelezwa mradi huo.

Mfanyabiashara wa pembejeo mjini Mpanda, Juma Machimu, anasema mwitikio wa wakulima kuhusu matumizi ya mifuko ya tabaka umeongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni.

Anasema mwaka 2024 aliuza mifuko 25 pekee, lakini mwaka 2025 idadi hiyo iliongezeka hadi mifuko 200. Kufikia mwaka 2026, tayari ameweza kuuza zaidi ya mifuko 500.

“Kadiri elimu inavyoongezeka, ndivyo wakulima wanavyozidi kuelewa umuhimu wa teknolojia hii. Wengi wanaanza kuona tofauti kati ya kuhifadhi mazao kwa kemikali na kutumia mifuko ya tabaka,” anasema.

Anaeleza kuwa ongezeko hilo limetokana na kampeni za elimu zinazotolewa na wadau wa kilimo, hususan Helvetas na SAT, ambazo zimewasaidia wakulima kuelewa faida za kuhifadhi mazao kwa njia salama zaidi.

**Gharama bado kikwazo**

Pamoja na mafanikio hayo, gharama ya mifuko ya tabaka bado ni changamoto inayotajwa mara kwa mara na wakulima na wafanyabiashara.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Mahindi Mpanda, Ashely Nduru, anasema teknolojia hiyo ina manufaa makubwa, lakini bei ya mifuko bado ni changamoto kwa watumiaji wengi.

“Mfuko mmoja wa tabaka unauzwa kati ya shilingi 4,500 na shilingi 5,000. Mfanyabiashara anayehitaji mifuko 300 analazimika kutumia zaidi ya shilingi milioni 1.5. Hii ni gharama kubwa kwa watu wengi,” anasema.

Inaendelea Uk. 20




*Baadhi ya mifuko ya tabaka ya PICS (Kinga Njaa) na SAFI iliyohifadhi mahindi, teknolojia inayowezesha wakulima kuhifadhi nafaka kwa usalama na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno.*

## Makala




***Mkulima kutoka Mpanda mkoani Katavi, Mwalimu Ezekiel Ulimbu, akishirikiana na kijana wake kujaza mahindi kwenye mifuko ya tabaka kwa ajili ya kuhifadhi mazao baada ya mavuno.***

# Teknolojia mpya...

Inatoka Uk. 19

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wakulima wanaendelea kutumia kemikali kuhifadhi mazao yao kwa sababu gharama zake zinaonekana kuwa nafuu zaidi kwa kipindi cha sasa.

Naye Elizabeth Kasuka, mkulima kutoka Mkoa wa Katavi, anaiomba serikali na wadau wa maendeleo kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za mifuko hiyo ili iweze kuwafikia wakulima wengi zaidi.

Anasema licha ya kutambua faida zake, wakulima wengi wadogo bado wanashindwa kumudu gharama za kuzinunua kwa kiwango kinachokidhi mahitaji yao.

**Afya ya mlaji kunufaika**

Mbali na kupunguza upotevu wa mazao, wataalamu wanaona teknolojia hiyo kama njia muhimu ya kulinda afya za walaji.

Meneja Mwandamizi wa Miradi kutoka SAT, Antusa Masawe, anasema tatizo la matumizi holela ya kemikali za kuhifadhi mazao limekuwa likihatarisha afya za wananchi kwa muda mrefu.

“Afya ya mlaji ni jambo muhimu sana. Mkulima anaweza kuhifadhi mazao yake, lakini mlaji hajui yametunzwa kwa namna gani. Ndiyo maana tunasisitiza matumizi ya teknolojia salama za uhifadhi,” anasema.

Anabainisha kuwa mifuko ya tabaka inaweza kutumika hata kuhifadhi mbegu za msimu unaofuata bila kuathiri ubora wake, mradi mazao yamekaushwa vizuri kabla ya kuhifadhiwa.

Inaendelea Uk. 21

# Teknolojia mpya...

Inatoka Uk. 20

Antusa anasema uhifadhi sahihi wa mazao pia husaidia kuhifadhi virutubisho vya asili vya nafaka na kuongeza muda wa matumizi ya mazao hayo bila kupoteza ubora wake.

### Teknolojia ya kidigitali

Ili kuwafikia wakulima wengi zaidi, wadau wa mradi wameanzisha mfumo wa kidigitali wa kuagiza na kusambaza mifuko ya tabaka.

Dkt. Recho Zakayo kutoka SUA anasema mfumo huo umesaidia kurahisisha upatikanaji wa mifuko kwa wakulima walioko maeneo mbalimbali.

Katika msimu wa mwaka 2026 pekee, zaidi ya mifuko 2,500 ilisambazwa katika Mkoa wa Katavi kupitia mfumo huo.

"Mkulima akishajiunga kwenye mfumo, tunapata taarifa zake pamoja na eneo alipo. Anaweza kuagiza mifuko na kulipia moja kwa moja au kupata kwa utaratibu wa mkopo na kulipa ndani ya siku kumi," anasema.

Hata hivyo, anataja changamoto za mtandao wa mawasiliano katika baadhi ya vijiji pamoja na umbali wa maeneo ya utekelezaji kuwa bado zinachelewesha huduma kuwafikia baadhi ya wakulima.

### Elimu yaenezwa

Mbali na usambazaji wa mifuko, mradi huo umewekeza katika kuwajengea uwezo wa kulima viongozi ili wawe mabalozi wa kueneza elimu kwa wakulima wenzao.

Meneja Msaidizi wa Miradi kutoka SAT, Muhammed Nkya, anasema mradi ulianza kama utafiti wa kutafuta njia bora za kuwashawishi wakulima kutumia teknolojia ya uhifadhi salama wa mazao.

Kwa sasa unatekelezwa katika wilaya za Gairo na Mvomero mkoani Morogoro pamoja na Chamwino na Kongwa mkoani Dodoma.

"Tumekuwa tukitoa mafunzo yanayoeleza kuwa upotevu wa mazao hauanzi baada ya mavuno pekee, bali unaweza kuanzia shambani, wakati wa uvunaji, usafirishaji na hata uhifadhi," anasema.

Katika Wilaya ya Mvomero, mkulima kiongozi mmoja anasema tayari amefikia zaidi ya kaya 300 kwa kutoa elimu kuhusu matumizi ya mifuko ya tabaka, huku akilenga kufikia kaya zaidi ya 1,000.

"Mpaka sasa zaidi ya mifuko 200 tayari imeagizwa na wakulima. Hii inaonyesha kuwa watu wameanza kuelewa umuhimu wa teknolojia hii,"anasema.

Naye Daudi Donathan, mkulima kiongozi kutoka Kibaigwa mkoani Dodoma, anasema matumizi ya mifuko hiyo yanampa mkulima uwezo wa kuhifadhi mazao kwa muda mrefu akisubiri bei nzuri sokoni bila kuhofia kuharibika.

"Mbali na kupata bei nzuri zaidi, mkulima na mfanyabiashara wanakuwa wamechangia kulinda afya za walaji kwa kuepuka matumizi ya kemikali za kuhifadhia mazao," anasema.

### Juhudi za serikali

Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Katavi, Faridu Abdallah, anasema mkoa huo unazalisha zaidi ya tani 600,000 za mazao ya chakula kwa mwaka, lakini kwa muda mrefu umekuwa ukikabiliwa na upotevu wa mazao unaofikia asilimia 40.

Anasema serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kujenga maghala ya kuhifadhi mazao na kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa za uhifadhi.

"Miaka mitatu iliyopita tulikuwa na maghala 200 pekee, lakini sasa tuna zaidi ya maghala 400 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 200,000 za mazao…"

"Sambamba na hilo, tunaendelea kuwajengea uwezo wakulima kutumia teknolojia za kisasa kama mifuko ya tabaka," anasema.

Kadiri matumizi ya mifuko ya tabaka yanavyoendelea kuongezeka, ndivyo matumaini ya kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno yanavyozidi kuimarika.

Kwa wakulima wengi, teknolojia hii si tu suluhisho la kuhifadhi mazao, bali ni fursa ya kuongeza kipato, kuimarisha usalama wa chakula na kulinda afya za walaji kwa njia endelevu.

Habari

# Tanzania kukabili dhamira ya Bunge la Ulaya



Na Mwandishi WETU

SERIKALI ya Tanzania imeingia kwenye mkakati wa kukabiliana na dhamira ya Kamati ya Mambo ya Nje ya Bunge la Ulaya, kuzuia kunufaika na ushirikiano wa nchi za bara hilo.

Dhamira hiyo sambamba na ile ya Kamati ya Maendeleo, inapendekeza kuwepo kwa zuio la ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU).

Mpango huo unatokana na kamati hizo kupitisha azimio la kusimamisha msaada wa maendeleo wa takribani Euro 156 milioni (zaidi ya shilingi bilioni 440) kwa madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu, kukosekana kwa utawala bora, kukandamizwa kwa demokrasia na uhuru wa maoni nchini Tanzania.

Kamati ya Bunge la Ulaya inayohusika na masuala ya mambo ya nje na ile inayohusika ma masuala ya maendeleo, zimepitisha kura ya mapendekezo ya kusitisha Mpango wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2025 kati ya Tanzania na Umoja huo.

Katika kura hiyo, mapendekezo ya kamati hiyo ya Bunge la EU ya kusitisha msaada wa kifedha kwa Tanzania yamepitishwa kwa kura 81, huku kura moja ikipinga, na wajumbe wanne hawakupiga kura.

Baada ya hatua hiyo, muswada huo unatarajiwa kupelekwa rasmi katika Bunge la EU kwa ajili ya kupigiwa kura mwishoni mwa mwezi huu wa Juni, 2026.

Iwapo Bunge litaridhia mpango huo, ina maana kuwa taasisi zinazohusika na mpango huo wa maendeleo zitaarifiwa kuhusu uamuzi huo na zenyewe zitapaswa kuutekeleza kwa kusitisha mpango huo.

**Serikali yatoa kauli**

Hatua hiyo ililazimisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutoa taarifa muda mfupi baada ya taarifa za kuwepo kwa azimio hilo.

Katika taarifa yake wizara ilikiri kupokea taarifa kuhusu kura hiyo inayolenga kusimamisha ushirikiano na msaada huo kwa Tanzania.

Hata hivyo, wizara ikawatoa hofu wananchi kwa kueleza kuwa kura hiyo haimaanishi kuwa Tanzania imefutiwa misaada hiyo na EU na kwamba suala hilo halijafikia mwisho.

Katika ufafanuzi wake, wizara ikasema kuwa kura hiyo ni sehemu ya taratibu za ndani za Bunge la Ulaya kufanya uamuzi na kuwa katika hatua hii, ni Kamati ya Mambo ya Nje na Kamati ya Maendeleo pekee zilizojadili na kupigia kura mapendekezo yanayohusu Tanzania.

Wizara ikasema hata hivyo mchakato huo bado haujakamilika. “Kwa mujibu wa taratibu za Bunge la Ulaya, mapendekezo yaliyopitishwa katika ngazi ya kamati yanapaswa kuwasilishwa kwenye Kikao cha Bunge zima la Ulaya, linalojumuisha zaidi ya wabunge 700, kwa ajili ya mjadala na uamuzi…”

“Hivyo basi, kura hiyo ni hatua moja tu katika mchakato unaoendelea na haiwakilishi msimamo wa mwisho wa Bunge la Ulaya kuhusu suala hili,” ilieleza taarifa ya wizara.

Inaendelea Uk. 23

# Tanzania kukabili...

Inatoka Uk. 22



Wizara hiyo ikasisitiza kuwa uhusiano kati ya Umoja wa Ulaya na nchi washirika wake, ikiwemo Tanzania, unaendeshwa kupitia Tume ya Ulaya, ambayo ndiyo chombo cha utendaji cha Umoja wa Ulaya.

"Kama ilivyo katika mifumo mingi ya kibunge, mapendekezo yanayopitishwa na kamati za kibunge au na Bunge lenyewe, huwasilishwa kwa taasisi husika za kiutendaji kwa ajili ya kuzingatiwa na kufanyiwa kazi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa," ilieleza taarifa hiyo," ilisema wizara.

Taarifa hiyo ilisisitiza kuwa kwa muktadha huo, mapendekezo yaliyopitishwa na kamati za Bunge hayapaswi kutafsiriwa kuwa ni uamuzi wa moja kwa moja unaobainisha mustakabali wa mahusiano kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya kwa kuwa suala hilo bado liko ndani ya taratibu za Umoja wa Ulaya na halijafikia hatua ya mwisho ya uamuzi.

Aidha, wizara ikauhakikishia umma wa watanzania kuwa uhusiano kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya unaendelea kuwa imara na unazidi kustawi katika maeneo mbalimbali yenye maslahi ya pamoja.

"Tanzania na Umoja wa Ulaya zinafurahia ushirikiano wa muda mrefu uliojengwa juu ya mazungumzo, ushirikiano na kuheshimiana, unaoungwa mkono na mifumo imara ya mashauriano iliyoanzishwa vyema…"

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuwa na dhamira ya kuimarisha zaidi ushirikiano wake wa muda mrefu na Umoja wa Ulaya kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili na kwa ajili ya kufanikisha malengo ya pamoja ya maendeleo," ilieleza taarifa hiyo.

**Kwa nini?**

Sababu zilizotolewa na Umoja wa Ulaya kuinyima pesa Tanzania zilielezwa kuwa ni mauaji ya raia yaliyofanyika Oktoba 29, 2025, kukosekana kwa uwajibikaji, kufungwa kwa kiongozi wa upinzani Tundu Lissu, ukandamizaji wa demokrasia, ukandamizaji wa uhuru wa habari na uhuru wa kutoa maoni.

Tayari Kamati ya Ulinzi na Mambo ya Nje ya Bunge la Tanzania imekataa mapendekezo ya kushirikiana na Bunge la Ulaya kufanya uchunguzi huru wa mauaji ya Oktoba 29.

**Masharti ya fedha za EU**

Fedha hizo zilizotarajiwa kutolewa kwa njia ya msaada na siyo mkopo, ni kwa ajili ya kusaidia miradi ya afya, elimu, maji na nishati.

Miongoni mwa masharti yaliyoainishwa na kamati hizo za bunge la EU ili kuruhusu kutolewa kwa fedha hizo ni iwapo tu Serikali ya Tanzania itakubali vyombo vya kimataifa kuchunguza mauaji ya Oktoba 29, kuachiwa kwa kiongozi wa upinzani, Tundu Lissu na wafungwa wengine wa kisiasa bila masharti yoyote.

Pia, Tanzania ikatakiwa kuacha kufungia/kuvitisha vyombo vya habari na kuruhusu uhuru wa maoni na kukubali kushirikiana na vyombo vya kimataifa kuchunguza matukio ya watu kutekwa na kupotea.

## Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# Uhusiano na Umma, kazi ya kusema au kusikiliza?

SIKU moja nilikuwa katika ukumbi mmoja wa mikutano nikisubiri kikao kianze, pembeni yangu aliketi ofisa mmoja wa serikali mwenye uzoefu wa kutosha katika utumishi wa umma.

Katika mazungumzo yetu ya kawaida akanitupia swali ambalo lilionekana rahisi, lakini mpaka leo bado nalifikiria. “Kwa nini wananchi wengi hawaamini taarifa za serikali hata pale taarifa hizo zinapokuwa sahihi?” Nilitabasamu kidogo. Nikajua kabisa lile halikuhitaji jibu la dakika moja.

Tatizo kubwa siyo kwamba serikali haisemi, serikali zetu zinasema sana na kila siku kuna taarifa kwa umma.

Kila wiki kuna uzinduzi, kila mwezi kuna ripoti na kila mwaka kuna mafanikio yanatajwa, lakini wakati mwingine kadri tunavyozidi kusema, ndivyo wananchi wanavyozidi kutaka kusikia zaidi.

Hapo ndipo nilipoanza kuelewa kwamba Uhusiano na Umma (PR) katika sekta ya umma siyo kazi ya kuzungumza tu, bali ni kazi ya kujenga imani.

Unaweza kuwa na mradi mzuri wa maji au kuwa na hospitali mpya au shule mpya, lakini kama wananchi hawaelewi kilichofanyika au hawajisikii kuwa sehemu ya mchakato, basi mafanikio hayo yanaweza kubaki kwenye makabrasha na ripoti.

Kuna wakati taasisi za umma zimekuwa zikilaumiwa kwa urasimu, mwananchi anaingia ofisini akiwa na shida moja, anatoka akiwa na shida tatu zaidi, anapofika nyumbani anasimulia alichokutana nacho.

Kesho yake jirani yake anasimulia alichokutana nacho, wiki moja baadaye taasisi nzima inajikuta imejengewa taswira mbaya kuliko hata uhalisia wake.

Tatizo la taswira ni kwamba haijengwi kwa siku moja na ikishajengeka vibaya, haiondoki kwa mkutano mmoja na waandishi wa habari, ndiyo maana kazi ya PR serikalini imekuwa ngumu kuliko watu wengi wanavyofikiri.

Sekta binafsi inaweza kuuza bidhaa, serikali inauza imani na bidhaa inapoharibika unaweza kuibadilisha, lakini imani ikiharibika, safari ya kuirejesha ni ndefu sana.

Isivyokuwa bahati zaidi tunaishi katika dunia ambayo kila mtu ana simu mkononi, zamani malalamiko yalibaki sokoni, kwenye vijiwe au ndani ya daladala, leo malalamiko yanafika kwa maelfu ya watu ndani ya dakika chache.

Mwananchi akikutana na huduma mbaya saa mbili asubuhi, saa mbili na dakika kumi tayari watu elfu kadhaa wameiona video hiyo.

Serikali ikijibu kesho yake, mara nyingi huwa imechelewa, haya ndiyo mazingira mapya ya Uhusiano na Umma.

Lakini pamoja na changamoto hizo, kuna jambo moja ambalo linanivutia sana, kila tunapozungumza kuhusu maendeleo, mara nyingi tunazungumzia barabara, reli, viwanja vya ndege na majengo marefu.

Mara chache sana tunazungumzia mawasiliano.

Wakati mwingine serikali inaweza kujenga daraja kubwa kabisa nchini, lakini ikashindwa kujenga daraja kati yake na wananchi na daraja hilo la pili ndilo muhimu zaidi kwa sababu mwisho wa siku, wananchi wanataka kuheshimiwa, kusikilizwa na kupewa taarifa sahihi.

Wanataka kuelewa kwa nini jambo limefanyika, siyo kusikia tu kwamba limefanyika.

Kadri dunia inavyobadilika, ndivyo kazi ya Uhusiano na Umma itakavyobadilika pia, teknolojia mpya zitakuja na akili mnemba zitakuja.

Mfumo wa mawasiliano utaendelea kubadilika. Lakini kuna jambo moja ambalo halitabadilika. Wananchi wataendelea kutafuta ukweli na taasisi za umma zitaendelea kutafuta njia ya kuwafikia wananchi hao.

Swali kubwa ni hili; je, tutatumia teknolojia mpya kuwasikiliza wananchi zaidi au tutaitumia kuzungumza zaidi? Kwa sababu wakati mwingine wananchi hawahitaji taarifa nyingine bali wanahitaji tu mtu wa kuwasikiliza. Na pengine hapo ndipo Uhusiano na Umma halisi inapoanzia.

***Mwandishi wa safu hii ni Mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***

Na Emmanuel JACOB



# Msongo kazini chanzo cha changamoto



UNACHELEWA kulala ukimalizia ripoti za ofisini, unawahi kuamka asubuhi huku kichwa kikiuma, na unakimbizana na foleni ili uwahi meza ya kazi.

Katika ulimwengu wa sasa wa ushindani, kufanya kazi kwa saa 55 au zaidi kwa wiki kumegeuka kuwa sifa ya kujivunia.

Lakini nyuma ya haya yote, kuna ukweli wa kutofisha uliojificha; mazingira ya kazi yenye 'presha' kubwa na mzigo unaozidi uwezo wako yanaweza kuwa hatari kiafya.

Unapokuwa chini ya msongo wa mawazo wa muda mrefu (burnout), mwili wako hauchoki tu, bali utendaji kazi wa mwili hubadilika pia. Homoni za cortisol na adrenaline inapoendelea kuzalishwa kwa wingi mwilini, huathiri mishipa yako ya damu na inaweza kupelekea shinikizo la juu la damu. Kibaya zaidi, hali hii hubadili jinsi unavyoishi.

Unapolemewa na akili, ule uamuzi wa busara wa kula chakula bora au kwenda kufanya mazoezi unakufa. Badala yake, unajikuta ukitafuta ahueni ya haraka haraka ama kunywa vikombe vingi vya kahawa, soda, vyakula vya mafuta, glasi za pombe zilizokithiri, au sigara, kwa kisingizio cha "kupunguza stress."

Kitendo hiki cha kutumia tabia hatarishi kiafya kama ngao dhidi ya msongo wa mawazo kinarahisisha safari ya mwili wako kuelekea kwenye ugonjwa hatari wa kiharusi "stroke".

Homoni za stress pia huvuruga mfumo wa chakula na kusababisha vidonda vya tumbo (ulcers), kiungulia, na kukosa choo. Kiakili, burnout inachochea matatizo makubwa ya afya ya akili kama sonona (depression), wasiwasi uliopitiliza (anxiety), na ukosefu wa usingizi wa muda mrefu (insomnia).

Mabadiliko ya mfumo wa mmeng'enyo na tabia mbaya za ulaji huongeza hatari ya unene uliopitiliza na kisukari cha ukubwani (Type 2 Diabetes), huku mwili ukikabiliwa na maumivu sugu ya misuli, mgongo, na kichwa yote yanayoshusha kabisa ufanisi wako wa kazi.

Ili kujinusuru, ni muhimu kuchukua hatua madhubuti: kuweka mipaka thabiti kati ya kazi na maisha binafsi, kujenga utaratibu wa kupima presha mara kwa mara nyumbani au kwenye vituo vya afya vilivyo karibu, kufanya mazoezi mepesi ili kushusha stress, na kuomba msaada wa kisaikolojia pale inapobidi.

Kumbuka, kampuni yako itatafuta mbadala wako mara moja ukiumwa; kulinda afya yako leo ndio uamuzi wa busara zaidi.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Ameandika Kitabu cha Mbinu za Kutibu Maumivu Sugu). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob***

Habari

# Olengurumwa asisitiza elimu, atoa angalizo kwa watetezi wa haki



Wakili Onesmo Olengurumwa

Na Mwandishi WETU

MRATIBU wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Wakili Onesmo Olengurumwa, amewataka watetezi wa haki za binadamu nchini kujiendeleza kielimu.

Akitoa salamu zake za mwisho jijini New York, Marekani baada ya kuhitimu mafunzo maalum ya miezi saba, Olengurumwa amesisitiza kuwa kazi ya utetezi wa haki kwa sasa inahitaji "watu walioshiba kielimu na mbinu za kisasa kupigania haki."

Aliwashauri watetezi hao wa haki za binadamu, kujiunganisha na taaluma za kitaalamu kupitia vyuo vikuu vikubwa duniani, ili kujenga weledi na mbinu mpya za kitaalamu zitakazosaidia kuhimili dhoruba za sasa za kiusalama na kisiasa.

Olengurumwa ambaye hivi karibuni alihitimu mafunzo ya Human Rights Advocates Program (HRAP) yanayoendeshwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Haki za Binadamu katika Chuo Kikuu cha Columbia, akiwa miongoni mwa wanaharakati wachache waliochaguliwa duniani kote.

Akielezea uzoefu wake binafsi wa jinsi ya kujiendeleza kielimu kulivyomsaidia kuongeza tija katika nchi, anasema amekuwa akitafuta kozi fupi fupi katika vyuo vikuu vikubwa duniani.

Sambamba na kuhimiza masuala ya elimu, Olengurumwa pia ametahadharisha asasi za kiraia duniani kote kuhusu mabadiliko ya maslahi ya mataifa makubwa – hasa kuhusu namna zinavyoweza kuwa imara na kuendelea na majukumu hata kama ufadhili unaweza kukosekana ama kuminywa kwa kiasi kikubwa.

"Kipindi hiki ni kigumu sana kufanya kazi ya haki za binadamu kwa sababu mtazamo na maslahi ya kidunia yamehama kutoka kwenye kulinda haki na kwenda kwenye masuala ya uwekezaji, biashara, na vita vya kijiografia…" "Ni wakati sasa ambao tunapaswa kuepuka kufanya kazi kwa kujitenga. Ni wakati ambao tunahitaji mshikamano wa kimataifa ili kukabili au kushughulikia baadhi ya changamoto hizi za kijiografia na kisiasa, au za kidunia, zinazoathiri haki za binadamu kwa mapana yake…"

"Hili ni jambo ambalo hatupendi kuona kundi fulani la watendaji likichukua hatua bila kuungana na wengine. Watendaji wa haki za binadamu wa ukanda wa kusini mwa dunia, wale wa kaskazini, na wa magharibi, sote tunahitaji kuungana pamoja na kukabiliana na changamoto hizi za sasa", amesema.

Katika mafunzo hayo, Wakili Olengurumwa aliungana na wanasheria na watetezi kutoka mataifa mengine katika mafunzo hayo adhimu ambapo washiriki walijifunza masuala mbalimbali ya mbinu za kisasa kukabili uonevu na kutetea haki za binadamu katika mazingira magumu.



Na Rashid MTAGALUKA

Hoja Yangu

# WhatsApp, TikTok, Facebook wahalifu wapya wa ndoa

TAARIFA ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dorothy Gwajima aliyoitoa wiki iliyopita, kwamba serikali ilipokea mashauri 49,573 ya ndoa kati ya Julai 2025 na Aprili 2026, imefungua mjadala mpana kuhusu sababu za migogoro ya ndoa nchini.

Ingawa changamoto za uchumi na malezi zinatajwa mara nyingi, lakini kuna swali moja ambalo jamii inaanza kujiuliza kwa sauti kubwa; je, mitandao ya kijamii imekuwa adui mpya wa ndoa za Watanzania?

Hii ni kwa sababu miaka michache iliyopita, migogoro mingi ya ndoa ilikuwa inahusishwa na matatizo ya kifedha, ulevi au migogoro ya kifamilia. Leo hii, simu janja imeingia katikati ya uhusiano wa wanandoa.

WhatsApp, Facebook, TikTok na Instagram zimekuwa sehemu ya maisha ya kila siku, lakini pia zinatajwa kugeuka kuwa chanzo cha migogoro mipya.

Katika mazingira ya sasa, mtu anaweza kuanzisha uhusiano wa siri akiwa ameketi sebuleni pamoja na mwenzi wake. Mazungumzo ya faragha, akaunti za siri na matumizi ya muda mwingi mtandaoni yamekuwa vyanzo vya shaka na migogoro katika familia nyingi.

Tatizo siyo teknolojia yenyewe, bali namna inavyotumiwa. Mitandao imeongeza fursa za mawasiliano, lakini pia imeongeza fursa za usaliti wa kihisia na kimapenzi.

Wataalamu wa saikolojia wamekuwa wakieleza kuwa uaminifu ndani ya ndoa huanza kupungua pale ambapo mmoja wa wanandoa anaanza kujenga ukaribu mkubwa wa kihisia na mtu mwingine kupitia mitandao.

Takwimu za serikali zinaonyesha kuwa maelfu ya mashauri ya ndoa yanaendelea kushughulikiwa huku mengine yakipelekwa mahakamani, jambo linaloonyesha ukubwa wa changamoto inayozikabili familia nyingi za Tanzania.

Athari zake zinaonekana pia kwa watoto. Serikali imewahi kueleza kuwa migogoro ya kifamilia ni miongoni mwa sababu zinazochangia watoto kukimbilia mitaani au kuishi katika mazingira yasiyo salama.




Kwa hiyo, tunapozungumzia kesi 49,573 za ndoa, hatupaswi kuangalia tu idadi ya mashauri yaliyofikishwa serikalini, ni vyema tukajiuliza kama jamii imejiandaa kukabiliana na changamoto mpya zinazoletwa na dunia ya kidijitali.

Mitandao ya kijamii siyo adui wa ndoa kwa asili. Lakini inapokuwa na nafasi kubwa kuliko mawasiliano ya ana kwa ana kati ya wanandoa, inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha migogoro.

Kazi iliyopo mbele yetu siyo kupiga vita teknolojia, bali kujenga matumizi yenye mipaka, uwazi na uwajibikaji ndani ya familia.

Kama takwimu hizi ni kengele ya hatari, basi moja ya ujumbe wake mkubwa ni kwamba ndoa za kisasa zinahitaji si tu upendo na uvumilivu, bali pia nidhamu ya matumizi ya teknolojia.

Bila hivyo, WhatsApp, TikTok na Facebook zinaweza kuendelea kuandikwa katika orodha ya sababu zinazoitikisa taasisi ya ndoa nchini Tanzania.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

# Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Utunzaji mazingira uzingatie afya

**Mhariri,**

JIJI la Dar es Salaam ni moja kati ya majiji yenye changamoto ya mazingira hasa maeneo ya kutupa takataka.

Kutokana na changamoto hiyo, yapo maeneo ambayo yanatumika kutupa taka, lakini sasa yameathiriwa na mvua na kusababisha mmomonyoko wa udongo. Eneo la Nyakasangwe, lililopo Kata ya Wazo Hill kuna mkondo mkubwa wa maji ambao umechangia kuta za mkondo huo kulika.

Katika kudhibiti athari hiyo, uongozi wa eneo hilo umelazimika kuelekeza magari ya kutupa takataka kumwaga katika Dampo la kwa Mzola ili kuzuia nyumba zilizo karibu zisiathirike.

Wazo hilo ni zuri ila inabidi eneo hilo liandaliwe kwa ajili ya kutunza takataka bila kuleta madhara kwa wakazi wa jirani. Viongozi pia wajenge utamaduni wa kukagua eneo hilo mara kwa mara, ili kuhakikisha takataka zinapofikishwa eneo husika, zinawekwa dawa ili kuzuia harufu mbaya na inzi, ambao wanaweza kuwa chanzo cha kusambaza magonjwa.

**Juma Hamis, Wazo Hill, Dar es Salaam.**

## Trafiki waheshimu muda wa abiria

**Mhariri,**

NIKIWA ni miongoni mwa wanaotumia usafiri wa umma, tumekuwa tukikutana na changamoto ya askari wa usalama barabarani.

Changamoto kubwa ni pale askari wanapokamata daladala na kuzuia kwa muda mrefu, huku ikiwa na abiria ambao wanahitaji kuwahi kwenye majukumu yao.

Utaratibu uko wazi kwamba kama gari ikikamatwa na kukutwa na kosa, kinachotakiwa ni kumuandikia kosa dereva.

Lakini utakuta askari anashilikia gari ikiwa na abiria hadi kwa nusu saa.

Kinachonisikitisha ni namna askari wanavyozuia gari bila kujali muda wa abiria wanaoupoteza huku wakiwachelewesha kwenye shughuli zao bila kujali madhila wanayowasababishia.

Kama gari ina matatizo, basi ni vyema iruhusiwe mapema ipeleke abiria kisha iendelee na taratibu nyingine.

**Bwisu Alphonce,**
**Mkazi wa Tegeta, Dar es Salaam.**

## Barabara Shule Maalum ya Samia itengenezwe

**Mhariri,**

HII ni mara ya pili nakuandikia kilio changu na wengine wengi tunaotumia Barabara ya Njeteni, iliyoko eneo la Kwembe, Ubungo Dar es Salaam.

Barabara hiyo inayoelekea Shule Maalum ya Wasichana ya Dar es Salaam, almaarufu – Shule ya Samia, ni mbovu mno na inahitaji matengenezo ya haraka kabla mvua hazijaanza kwani ndiyo itashindwa kupitika kabisa.

Miaka nenda-rudi, sisi wakazi wa maeneo hayo, tunaotumia barabara hiyo, ni kama tumetelekezwa na watendaji wanaohusika na barabara, tumepiga sana kelele kuomba itengenezwe kwa kiwango hata cha changarawe, lakini hakuna anayejali.

Tunaomba sasa wakubwa wetu wa Dar es Salaam, na hasa kupitia Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, wizara watusaidie ili na sisi tuone matunda ya kuwa Watanzania.

**Rashid Hamduni Hassan,**
**Eneo la Kwahovyo, Kwembe**

# Ni ugonjwa wapinzani kuegemea ajenda za CCM

Na Philipo MWAKIBINGA

MOJA ya changamoto ambazo vyama vingi vya upinzani Afrika hukumbana nazo ni kushindwa kutengeneza ajenda zao za kisiasa na badala yake kujikuta vikitegemea ajenda za chama tawala.

Hali hii imekuwa ikijitokeza mara kwa mara nchini Tanzania, ambapo mara nyingi mijadala mikubwa ya upinzani huibuka kufuatia matukio yanayohusishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Tatizo la mkakati huu ni kwamba chama kinachotengeneza ajenda ndicho kinachodhibiti uwanja wa mchezo wa kisiasa.

Kama CCM ndiyo inayobuni hoja, kuzindua miradi, kufanya mikutano mikubwa au kuibua mijadala inayovuta hisia za wananchi, upinzani unapokimbilia kujibu kila tukio unajikuta unacheza mchezo ulioandaliwa na mwingine.

Katika siasa za kisasa, wataalamu wa mawasiliano ya kisiasa huamini kwamba chama chenye uwezo wa kuweka ajenda ya mjadala wa umma huwa na faida kubwa kuliko chama kinachojibu ajenda za wengine.

Ndiyo maana mara nyingi wananchi hukumbuka nani aliyeanzisha mjadala kuliko nani aliyeujibu.

Iwapo chama tawala kingekuwa na mkakati wa kuhamisha mjadala wa umma kutoka eneo moja kwenda jingine, kingehitaji tu kuibua tukio au hoja mpya inayovuta hisia za wananchi.

Upinzani ambao hauna ajenda zake za kudumu ungejikuta ukiacha masuala yake ya msingi na kukimbilia kujadili tukio hilo jipya. Matokeo yake ni kupoteza muda, nguvu na umakini wa kisiasa.

Ndiyo maana mara nyingi tunaona hoja za upinzani zikibadilika kulingana na matukio yanayotokea ndani ya CCM, badala ya kuendeshwa na sera, mipango na maono yao




wenyewe. Leo wanazungumzia jambo moja, kesho jingine, kulingana na kile kilichotokea upande wa chama tawala.

Kwa chama chochote kinachotaka kushinda uchaguzi, mkakati wa kutegemea makosa, kauli au matukio ya mpinzani wake hauwezi kuwa mbadala wa kuwa na ajenda yake ya maendeleo, uchumi, elimu, afya na ustawi wa wananchi.

Wananchi wanataka kusikia mbadala wa uongozi, siyo maoni kuhusu kila tukio linalotokea kwa mpinzani.

Kwa hiyo, ikiwa kweli upinzani unataka kujijenga kama mbadala wa CCM, unapaswa kuwekeza zaidi katika kutengeneza ajenda zake kuliko kusubiri matukio ya CCM ili upate cha kuzungumzia.

Vinginevyo, utaendelea kuwa mfuasi wa ajenda za wengine badala ya kuwa mtengeneza ajenda za taifa.

Chama kinachotawala mjadala wa kisiasa siyo lazima kiwe na sauti kubwa zaidi, bali ndicho kinachowafanya wengine wazungumzie mambo yake kila siku.

Ndiyo maana kuna tukio linaweza kutokea usiku kwa mwana CCM halafu asubuhi mapema kiongozi mkubwa wa upinzani akamsafisha haraka mwanachama huyo na kumkaribisha ndani ya chama cha upinzani ambaye hapo mwanzo alionekana tatizo kwa mujibu wa kauli zao.

■ Mtazamo Binafsi

# Ujio wa meli ya mafuta Zanzibar historia mpya ya uchumi wa bahari


*Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi*

**Na Steven MMBOGO**

TUNAWEZA kujiuliza swali hili; je, Zanzibar inaandika ramani mpya ya uchumi wa bahari, huku Tanzania Bara ikiendelea kubeba miradi mfu?

Mwishoni mwa Mei 2026, Zanzibar ilishuhudia tukio ambalo kwa macho ya kawaida linaweza kuonekana habari ya kawaida ya biashara ya mafuta.

Meli kubwa ya kimataifa kutoka Saudi Arabia ilitia nanga katika Bandari Jumuishi ya Mangapwani na kushusha zaidi ya lita milioni 36 za petroli, dizeli na mafuta ya ndege moja kwa moja huko Zanzibar.

Hili lilikuwa tukio la kwanza la aina yake katika historia ya visiwa hivyo. Kwa jicho la mchambuzi wa sera za uchumi na maendeleo, tukio hili ni zaidi ya ujio wa mafuta.

Tukio hili ni ishara ya mabadiliko makubwa ya kimkakati yanayoendelea Zanzibar; mabadiliko yanayoweza kubadili nafasi yake ndani ya Muungano, ndani ya Tanzania na hata katika uchumi wa Bahari ya Hindi.

Swali muhimu siyo kwamba mafuta yamefika Mangapwani, jibu ni kwamba, Zanzibar imeamua kuwekeza nguvu kubwa katika miundombinu ya bandari, nishati na biashara ya kimataifa wakati maeneo mengi ya Tanganyika bado yanahangaika na miradi mikubwa iliyobaki kuwa "miradi mfu"?

Zanzibar inajenga uchumi wa miundombinu, siyo uchumi wa matumaini. Kwa miaka mingi, Zanzibar imekuwa ikitazamwa kuwa inategemea zaidi uchumi wa utalii, biashara ndogo ndogo na huduma.

Lakini chini ya uongozi wa Rais Hussein Ali Mwinyi, kuna dalili za wazi kuwa Zanzibar imeanza kuhamia katika kile wachumi wanaita ukuaji wa uchumi unaosukumwa kwanza na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu.

Mangapwani siyo bandari tu, bali ni sehemu ya mkakati mpana unaolenga kutatua changamoto tatu ambazo Serikali ya Zanzibar imezitambua kama vizuizi vikuu vya ukuaji wake ambavyo ni pamoja na msongamano wa bandari, upatikanaji wa nishati, uhifadhi na usambazaji wa mafuta. Hapa ndipo umuhimu wa ujio wa meli ya mafuta kutoka Saudi Arabia unaonekana.

Kwa mara ya kwanza, Zanzibar imeanza kuvunja utegemezi wake wa kihistoria wa kupokea mafuta kupitia Tanga, Dar es Salaam au Mombasa kabla ya kuhamishiwa visiwani kwa gharama kubwa zaidi.

Katika lugha ya uchumi, hii ni hatua ya kuondoa kile kinachoitwa gharama za miamala ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikidhoofisha ushindani wa uchumi wa Zanzibar.

Inaendelea Uk. 31



# Ujio wa meli...

Inatoka Uk. 30

Tukio la Mangapwani linaibua mjadala mpana zaidi kuhusu miradi mfu iliyogubikwa na historia ya maendeleo ya Tanganyika.

Zaidi ya miaka 40, Tanzania Bara imekuwa na orodha ndefu ya miradi mikubwa iliyotangazwa kwa mbwembwe, lakini ikashindwa kufikia matarajio yake.

Mfano maarufu ni Bandari ya Bagamoyo. Zaidi ya muongo mmoja, Watanzania waliambiwa kuwa bandari hiyo ingekuwa moja ya bandari kubwa zaidi Afrika Mashariki.

Mabilioni ya dola yalizungumzwa, wawekezaji wakatajwa, mipango ikatangazwa, lakini hadi leo, Bagamoyo bado haijawa injini ya uchumi ambayo iliahidiwa.

Hali kama hiyo imewahi kuonekana katika maeneo mengine mengi ya viwanda maalumu, miji ya kisasa, maeneo ya usafirishaji na hata baadhi ya miradi ya reli na bandari ambazo zilianza kwa kasi kubwa kisiasa kuliko kiuchumi.

Tatizo kubwa la miradi mingi ya Tanganyika limekuwa moja; kuzalisha maono kabla ya kujenga mfumo wa utekelezaji.

Kwa upande wa Zanzibar, kinachoonekana sasa ni tofauti, badala ya kuanza na hadithi kubwa za kisiasa, inaonekana wameanza na kuondoa vizuizi vinavyokwamisha biashara.

Vizuizi hivyo ni pamoja na bandari kwanza, uhifadhi wa mafuta kwanza, miundombinu ya usafirishaji kwanza, nguvu ya umeme kwanza kisha biashara ifuate. Hii ndiyo falsafa iliyotumiwa na nchi nyingi za Asia Mashariki zilizoibuka kiuchumi.

**Je, Zanzibar kuwa kitovu cha mafuta**

Kauli ya viongozi wa Zanzibar kwamba lengo ni kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha kikanda cha mafuta haipaswi kuchukuliwa kama maneno ya kisiasa tu.

Takwimu zinaonyesha kuwa Zanzibar hutumia takribani lita milioni 30 za mafuta kwa mwezi, lakini mipango ya hifadhi inayojengwa inazidi mahitaji hayo kwa kiwango kikubwa.

Kwa mantiki ya biashara, hujengi uwezo wa kuhifadhi mafuta kwa kiwango kikubwa kuliko matumizi yako ya ndani isipokuwa una malengo ya kuhudumia soko pana zaidi.

Hii inaashiria uwezekano wa Zanzibar kujipanga kuwa kituo cha kuhifadhi, kupokea na kusambaza mafuta kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Bahari ya Hindi.

Inaendelea Uk. 32

Mtazamo Binafsi

# Ujio wa meli...

Inatoka Uk. 31

Iwapo hilo litatimia, Zanzibar inaweza kujikuta ikifanya kile ambacho zamani kilifanywa na bandari za Fujairah katika Umoja wa Falme za kiarabu (UAE) au Singapore katika Asia, kuwa kitovu cha biashara ya nishati.

Ni safari ndefu, lakini ishara za mwanzo zinaonekana, uchumi wa bluu unaanza kuonekana kwa vitendo.

Kwa miaka kadhaa, dhana ya uchumi wa bluu imekuwa ikitajwa Zanzibar. Wengi waliiona kama kauli ya kisiasa yenye mvuto mzuri lakini isiyoeleweka vizuri.

Mangapwani huenda ikawa shahidi wa kwanza mkubwa kwamba Uchumi wa Bluu ya Zanzibar unaanza kutafsiriwa katika miradi halisi ambayo ni pamoja na bandari mpya, maghala ya mafuta, vituo vya usafirishaji, huduma za mipango na biashara za kimataifa. Hivi vyote ni sehemu ya uchumi wa bahari.

Kwa maneno mengine, Zanzibar inaonekana kujaribu kutumia jiografia yake kama mtaji. Na katika historia ya maendeleo ya dunia, nchi na maeneo yaliyofanikiwa zaidi mara nyingi ni yale yaliyogeuza eneo lao la kijiografia kuwa faida ya kiuchumi.

Singapore ilifanya hivyo, Dubai ilifanya hivyo, Panama ilifanya hivyo, sasa Zanzibar inaonekana kujaribu kufanya hivyo kwa kiwango chake.

**Athari kwa Muungano**

Kuna hoja nyeti lakini muhimu ambayo wachambuzi hawapaswi kuikwepa.

Kwamba kadri Zanzibar inavyojenga uwezo wake wa moja kwa moja wa kupokea mizigo, mafuta na uwekezaji wa kimataifa, ndivyo utegemezi wake wa kiuchumi kwa miundombinu ya bara unavyopungua. Hii si hoja ya kisiasa, bali hoja ya kiuchumi.

Kwa miaka mingi, Dar es Salaam, Tanga na Mombasa zilikuwa lango kuu la Zanzibar. Sasa Zanzibar inaonekana kujenga lango lake yenyewe. Hali hii inaweza kuleta ushindani mpya wa kiuchumi ndani ya Tanzania.

Lakini pia inaweza kuleta ushirikiano mpya. Swali litakuwa je, Serikali ya Muungano itaona ukuaji wa Zanzibar kama nyongeza ya uwezo wa taifa au kama ushindani wa ndani wa bandari na biashara.

**Historia inafundisha nini?**

Pamoja na matumaini yote, tahadhari inahitajika. Afrika imewahi kushuhudia miradi mingi mikubwa ya bandari ambayo ilitangazwa kama mabadiliko ya kihistoria lakini baadaye ikashindwa kuvutia biashara ya kutosha.

Bandari kubwa pekee hazitoshi, kinachohitajika ni mazingira mazuri ya biashara; sera thabiti; usimamizi wenye weledi; mtaji wa ndani na uwezo wa kuvutia meli na biashara kwa muda mrefu.

Ikiwa Zanzibar itashindwa kujenga mfumo huo, Mangapwani inaweza kuishia kuwa mradi mwingine mkubwa wa miundombinu usiozalisha thamani iliyokusudiwa.

Lakini ikiwa itaweza kuunganisha bandari, nishati, biashara, viwanda na uwekezaji wa kimataifa katika mfumo mmoja, basi miaka 20 ijayo inaweza kuikuta Zanzibar ikiwa katika nafasi tofauti kabisa ya kiuchumi kuliko ilivyo leo.

Tuhitimishe makala haya kwa kusema kuwa ujio wa tenki la kwanza kutoka Saudi Arabia si habari ya mafuta pekee, ni ishara ya mwelekeo mpya wa Zanzibar.

Ni dalili kwamba Zanzibar imeamua kuwekeza katika miundombinu inayoweza kuibadilisha kutoka uchumi wa huduma za utalii kwenda uchumi wa huduma, biashara na nishati.

Na pengine somo kubwa kwa Tanganyika si kuhusu mafuta yaliyoshushwa Mangapwani, bali maendeleo ya kisasa hayajengwi kwa kutangaza miradi mikubwa. Yanajengwa kwa kuondoa vizuizi vya biashara, kujenga miundombinu yenye tija na kuhakikisha kila mradi unaingia moja kwa moja katika mnyororo wa uzalishaji wa uchumi.

Iwapo Mangapwani itafanikiwa, inaweza kuwa si tu ushindi wa Zanzibar, bali pia ushahidi kwamba Afrika Mashariki inaweza kujenga vituo vipya vya uchumi bila kusubiri miujiza ya kisiasa.

Na hapo ndipo mjadala halisi unaanza. Mangapwani inaweza kuwa bandari ya mafuta leo; lakini kesho inaweza kuwa alama ya kuzaliwa kwa Zanzibar mpya ya kiuchumi.

# Habari katika picha



*Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Makamu wa Rais Balozi, Dkt. Emmanuel Nchimbi na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Asha-Rose Migiro baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam akitokea Russia juzi. (Picha na Ikulu).*



*Polisi Kata wa Mwakakati, Robert Kasunga, akizungumza na wazazi wa wanafuzi wa Shule ya Msingi Tanganyika iliyopo Wilaya ya Momba, Songwe kuhusu kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na aina nyingine za unyanyasaji juzi. (Picha na Issa Mwadangala).*



*Barabara ya kuingia Soko la Ndizi Mabibo ikiwa imejaa matope kutokana na kutofanyiwa matengenezo kwa muda mrefu, jijini Dar es Salaam jana. (Na Mpigapicha Wetu).*



*Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia viongozi na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha RUDN baada ya kutunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima.*



*Wafanyabiashara ndogo katika stendi ya daladala Mbezi ambao wamekaidi agizo la kupanga bidhaa sehemu za abiria kusubiria magari wakiendelea na shughuli zao kama walivyokutwa, Dar es Salaam jana. (Na Mpigapicha Wetu).*

# Marathoni

NHC
BUILDING OUR NATION
EB MARITIME GROUP
Total Logistics Network
KILIMANJARO
TANZANITE
Royal Gin
AZANIA BANK
KALUBA
montage
ITV
RADIO One
ayo TV
RBS
4J'S FITNESS center
ZAK'S PREMIUM
SGA SECURITY



## Mitindo & Urembo

# Yafahamu mavazi mazuri ya wanawake wanene



BAADHI ya wanawake wanene wamekuwa wakihangaika kupata aina ya nguo za kuvaa kutokana na maumbo yao.

Wengi wao wamekuwa wakikosa uhuru wa kutoka 'out' na wengine wakijikuta wakivaa nguo pana ili kuficha maumbo yao.

Zifuatazo ni tips ambazo zitakusaidia kuchagua nguo hasa kwa wale wanene;

*Kabla ya kuchagua nguo ni lazima ufahamu mwili wako una unene wa aina gani, ikiwa ni mnene na tumbo kubwa basi ni bora kuvaa gauni ambalo litasaidia kukuweka vizuri.

*Kama wewe ni mnene na una matiti makubwa; pendelea kuvaa nguo zenye v-shape ambayo husaidia kuficha ukubwa wa matiti na kuonekana maridadi, lakini zingatia kuvaa sidiria nzuri ambayo itakukaa vizuri.

*Kwa mwenye hips pana, anashauriwa kuvaa nguo zinakazomfanya asionyeshe sana hips zake tofauti na yule ambaye hana.

*Zingatia pia uchaguzi wa rangi ya nguo husaidia kupunguza au kuongeza umbile, kuna rangi hukufanya ukawa mnene au mwembamba sana. Kwa mfano; nguo zenye mistari ya kulala siyo nzuri kwa watu wanene maana hutanua miili yao.

Lakini pia rangi za giza hupunguza mwonekano wa unene wakati rangi za mwanga huangaza na kufanya mtu aonekane sana.

**Zingatia haya**

*Chagua rangi za nguo nyeusi na nyeupe iliyochanganywa ni nzuri zaidi.

*Vaa viatu vinavyoendana na mwili wako sio lazima kuvaa kiatu kirefu wakati mwili wako hauhimili mikikimikiki ya kiatu kirefu, flatshoes pia hupendeza zaidi kwa mtu mnene.





# Harmonize azipongeza WCB, Kings Music

Na Mwandishi WETU

MSANII wa Bongo Fleva, Rajab Abdul Kahali maarufu Harmonize, amesema mfuatiliaji yeyote wa muziki nchini hawezi akaacha kuzisifia 'label' mbili ya WCB na Kings Music.

Akizungumzia mazingira ya wasanii wanapotoka kwenye label hizo hutamani kufanya kazi na upande mwingine haraka iwezekanavyo ili kupata mashabiki wa upande mwingine.

Amesema kwake ilikuwa tofauti hakutaka kufanya kolabo kipindi hicho lakini sasa imepita miaka sita hadi kufanya kazi na wasanii wote wakubwa wa Afrika Mashariki.

Aidha amesema kuwa kwa sasa amefanya wimbo mzuri "utanionea" akishirikiana na Ali Kiba kutoka Kings Music na pia wamenyanyua mapanga.



# Darassa anusurika kifo chanzo ni chakula

Na Mwandishi WETU

MSANII wa muziki wa kufokafoka - rap nchini, Darassa amenusurika kifo baada ya kupata changamoto ya ghafla ya kiafya inayodaiwa kusababishwa na chakula alichokula.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Darassa amemshukuru Mungu na madaktari na wauguzi waliomuwahi na kumpa matibabu ya haraka baada ya kukimbizwa hospitali.

"Hali yangu ilibadilika ghafla na kuwa mbaya kiasi cha kutishia maisha yangu chanzo kikiwa ni chakula nilichokula, namshukuru Mungu na madaktari sasa naendelea vizuri," ameandika.


Bati/ Mtu, Mtu Bati
HATUCHOKI!
Changia kupitia
NMB A/C NO 31910046325
ELCT KARAGWE IRON SHEET PROJECT
CRDB A/C NO 0150764151900
UWAKILI PROJECT ELCT KAD
Mawasiliano:
0754 742 423
Askofu Benson K Bagonza



# Haya yazingatiwe haraka kupaisha Serengeti Boys

**Na Mwandishi WETU**

UHAKIKA ni kwamba Timu ya Taifa ya Vijana, Serengeti Boys imeweka mizania ambayo ikifuatwa, Tanzania inaweza kufika mbali kwenye soka.

Serengeti Boys wameonyesha kuwa Tanzania ina vipaji, lakini vipaji peke yake havitoshi bila mfumo madhubuti wa kuvilea, kuvilinda na kuviandaa kushindana na dunia.

Kufika fainali ya Kombe la Afrika kwa Vijana – chini ya miaka 17 (Afcon - U17) na kutolewa na Senegal kwa mikwaju ya penalti siyo sababu ya kulia kwa muda mrefu, bali ni mwito wa kitaifa wa kuanza maandalizi makubwa zaidi kuelekea Kombe la Dunia kwa Vijana.

Serikali, kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na wadau wa michezo, wanapaswa kuona mafanikio ya Serengeti Boys kuwa ni uwekezaji wa taifa, siyo tukio la msisimko wa siku chache.

Hawa vijana wameonyesha ujasiri, nidhamu na uwezo wa kupambana na mataifa makubwa ya soka Afrika. Kinachohitajika sasa ni kuwapa mazingira bora zaidi; kambi za muda mrefu, mechi za kirafiki za kimataifa, wataalamu wa saikolojia ya michezo, lishe sahihi, madaktari, wachambuzi wa viwango na makocha wa viungo.

Ieleweke kwamba michuano ya Kombe la Dunia siyo mashindano ya kubahatisha. Ni jukwaa la kasi, akili, mbinu na maandalizi ya kisayansi.

Timu zinazofanya vizuri huanza safari mapema; haziwapeleki vijana uwanjani kwa matumaini pekee. Ndiyo maana Serengeti Boys wanahitaji mpango maalumu wa serikali, wenye bajeti inayojulikana, ratiba inayofuatiliwa na tathmini ya kila hatua.

Ni vyema wakati wa maandalizi, kila mchezaji ajulikane anaendeleaje kiafya, kiufundi, kimasomo na kisaikolojia.

Jambo jingine muhimu ni kuhakikisha mafanikio haya hayageuki sherehe ya muda mfupi. Mara nyingi tunapofanikiwa kwenye michezo, tunapiga picha, tunatoa pongezi na baadaye tunasahau kazi ngumu inayofuata.

Safari hii isiwe hivyo, lazima kuwe na kamati ndogo ya kitaalamu inayoripoti kila mwezi juu ya maandalizi, changamoto, majeruhi, vifaa, mechi za kujipima na maendeleo ya kila mchezaji.

Pia, klabu za ndani zinapaswa kupewa wajibu wa kuwalinda na kuwaendeleza vijana hawa. Ni hatari kwa taifa kutumia nguvu kubwa kuibua vipaji, halafu vikapotea kwa kukosa mwongozo, mikataba bora au malezi ya kitaalamu.

Wazazi, shule, akademi na viongozi wa soka waunganishwe kwenye mfumo mmoja wa malezi. Hapa ndipo Tanzania inaweza kujenga kizazi kipya cha wachezaji wanaoelewa thamani ya nidhamu, elimu na taaluma.

Ushindi mkubwa zaidi wa Serengeti Boys siyo tu kufika fainali, bali kutufanya tuamini kwamba Tanzania inaweza. Sasa imani hiyo isiachwe ipotee kwenye hotuba na pongezi za mitandaoni.

Serikali iongeze nguvu, fedha, ufuatiliaji na uzito wa kitaifa katika maandalizi. Tukiwatayarisha vizuri, hawa vijana wanaweza kwenda Kombe la Dunia siyo kuwa washiriki wa kujifunza tu, bali taifa lenye ndoto halisi ya kushindana, kushangaza dunia, kuhamasisha watoto wengi kupenda soka na kuandika ukurasa mpya wa soka la Tanzania.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION